


WAKATI WA

KANISA LA FILADELFIA

 Ndugu alienda akaniletea sambusa kubwa moto ya cheri. Nawaambia, kudokeza kuna faida. Naye akasema, “Jamani. . .” Vipi kuhusu hilo, Ndugu Neville? Huyo hapo. Mnaona? Inaonekana kana kwamba sambusa ya cheri kidogo inapendwa. Ni nzuri sana. Ni kama tu ninavyosema wakati ukila sambusa ya cheri, sasa, wakati mwingine unapata mbegu. Sasa, si—siitupilii mbali sambusa, ninatupa tu hiyo mbegu na kuendelea kula sambusa ya cheri.

² Hivyo ndivyo ninavyotaka mfanye kuhusu jumbe hizi. Ukifikia. . . Ambataneni moja kwa moja nami, unapofikia kitu ambacho huwezi—huwezi kumeng’anya vizuri sana, mbona, vema, ninii tu. . . usitupilie mbali kitu hicho chote, tupa tu sehemu hiyo (hiyo mbegu), na uendelee tu kuila hiyo sambusa. Mbona, mara ukijifunza. Uh-hum.

³ Wakati wewe. . . Je, mnapenda kuku, kuku wa kukaangwa? Karibu kila mtu anapenda. Vema, basi, wakati unapokula kuku, ukifikia mfupa, hutupi kuku, unatupa tu mfupa. Hiyo si ni kweli, Pat? Unatupa tu mfupa, unaendelea kula kuku.

⁴ Vema, tuna furaha kwa sababu kwamba tunaweza kula Chakula kisicho na mfupa wala mbegu ndani Yake. Mikate myembamba ilishuka kutoka Mbinguni, inayoitwa “Mana,” inafunika kila mahali kwa utamu wa Mbinguni.

⁵ Mnajua, ninaamini ilikuwa ni Daudi aliyesema wakati mmoja, “Ladha yake ni kama asali kwenye mwamba.” Ninaamini mshairi alisema, “Ilikuwa ni Asali kwenye Mwamba.” Loo, ndugu yangu, umeonja ninii. . . uone ninii. . . kama. . . ladha yake ni kama asali kwenye mwamba. “Asali kwenye Mwamba, ndugu yangu.” Hivyo ndivyo ilivyo.

⁶ Sasa, mwajua, ni—nilishangaa wakati mmoja kile hilo lilichomaanisha, “asali kwenye mwamba.” Nami nikawazia, “Vema, labda walipata mzinga wa nyuki wakati mmoja mwambani.” Lakini nilipolifuatilia, nilipata uvuvio kidogo juu yake. Mimi. . . Sio wakati huo niliokuwa nikilitafuta, bali baadaye nilikuta kwamba kila mmoja wa hao wachungaji aliyekuwa na kondoo. . . Kuna jambo fulani kulihusu, mwajua, miili yetu imeumbwa kutokana na mavumbi ya nchi. Kila—kila kiumbe kilicho hai kinatoka ardhini. Basi kulikuwako na hawa wachungaji, waliamini ya kwamba chokaa ilimsaidia kondoo wakati akiwa na shida, mwajua, mgonjwa, ama kitu kingine. Walimtaka aurambe mwamba. Mmewaona kondoo wakifanya

hivyo, wanaenda na kuuramba mwamba. Basi kuwafanya kondoo waurambe mwamba, wangemwaga asali kidogo juu ya mwamba. Ndipo basi kondoo angeenda kuiramba hiyo asali, naye angepata na mwamba pia, mnaona, wakati—wakati akiiramba hiyo asali.

⁷ Vema, tuna mfuko mzima wa maandiko uliojaa Asali hapa. Tutaiweka kwenye Mwamba, si juu ya kanisa lolote; juu ya Mwamba, Kristo Yesu. Basi ninyi kondoo anzeni kuiramba sasa, na hakika m—m—mta—mtapata afya mara moja. Shida zote za dhambi zitakwisha utakaporamba—utakapouramba Mwamba. Hivyo tu ndivyo unavyopaswa kufanya.

⁸ Jambo fulani kuhusu mwamba ulio na uponyaji kwake, uponyaji. Katika siku zilizopita, kabla hawajapata chanjo za kichaa cha mbwa, walikuwa na kile walichoita “jiwekichaa.” Wakati mtu alipoumwa na mbwa mwenye kichaa, mbona, walimweka juu ya hili jiwekichaa. Na sasa, kama hilo jiwekichaa . . . Kama alinata kwenye hilo jiwekichaa, alipona; kama halikunata, basi mgonjwa huyo alikuwa hali mbaya sana, a—angekufa.

⁹ Kwa hiyo hivyo ndivyo ilivyo leo hii. Kuumwa kubaya sana nikujuako si kwa mbwa kichaa, bali ni ibilisi. Nasi tuna Jiwe kwa ajili yake, Mwamba wa Miaka. Ushikilie tu. Mradi tu umeushikilia, utapona. Wala kamwe usiuachilie na kurudi nyuma, endelea tu kushikilia. Ushikilie, na—nawe uta—utakuwa sawa.

¹⁰ Sasa kabla hatujaingia kwenye somo letu la usiku, basi—basi tunataka kusimama kwa dakika moja tu, tukiweza, kwa maombi mafupi.

¹¹ Wewe si dada ya Robert Daugherty, sivyo? Hapa. Alinipigia simu jana, ninaamini ndivyo, nami nilikuwa nikizungumza juu ya yeye kutaka kuombewa. Na si—sikujuu, kidogo unafanana naye, sikujuu kama ni wewe ama la. Nilikuona hapa jana jioni.

¹² Sasa, ni wangapi wanaotaka kukumbukwa mbele za Mungu, ama mnaotaka Mungu awakumbuke, hasa? Ninii tu . . .

¹³ Baba yetu wa Mbinguni, kama—kama vile maskini kiongozi wetu wa nyimbo huko Chicago alivyo zoea kuimba, “Nikumbuke wakati machozi yanapotiririka,” Bwana, nikumbuke sasa. Katika wakati wa kufa, katika . . . kote maishani, tunakutaka utukumbuke, Bwana. Tukumbuke si kama wenye dhambi, jinsi tulivyo, bali tunataka utukumbuke kama Wakristo wanaoungama; kwamba tumemkubali Yesu Kristo, Mwanao, na Mwokozi wetu, kwa ajili ya ninii yetu . . . awe ridhaa yetu kwa ajili ya dhambi zetu. Kwamba, tunajua ya kwamba hiyo ndiyo ninii pekee—nafasi pekee tuliyo nayo, barabara pekee, njia pekee ya wokovu. Si kupitia kwa kanisa lolote wala kwa njia zingine zote za kujitengezea, wala dhehebu lolote, bali kwa Yesu Kristo, na Yeye pekee.

14 Kwa hiyo tunakaribia katika Jina Lake usiku wa leo, tukiomba kwamba utatubariki tunapokusanyika pamoja kulisoma Neno Lako na kujua yale uliyotuwekea akiba, kwa ajili ya usiku wa leo. Tupate kuijenga miili ye—yetu ya kiroho ifanyiike Kanisa changamfu. Kanisa ambamo ungeweza kuishi, na kutembea ndani yake, na kujisikia umeridhika, ukitembea miongoni mwa watu Wako, ukitwambia la kufanya, na kujua ya kwamba tungelifanya mara moja.

15 Nasi tunakupenda, Baba, bali tunajua bado hatuko kabisa kwenye hali ambayo ungeweza kunena kupitia sisi jinsi tu ungependa. Kwa hiyo tunaomba ya kwamba utatutahiri, hiyo ni kusema, ukatilie mbali ujinga huu wote, nyama yote ya ziada kutoka kwetu usiku wa leo, tupate kujiweka wakfu kabisa Kwako, ili kwamba uweze kututumia wakati wowote. Nasi tunaomba ya kwamba wakati huo utakuwa ni usiku wa leo, Baba, ambapo utatutumia kuvileta hivi vibamba kutoka kwenye Biblia na kuvipiga msasa na kuwawezesha watu waone uakisi wa Kristo katika wakati huu mkuu wa kanisa. Tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

16 Sasa, tumekuwa na nyakati za kanisa sasa, kote kote mpaka wakati wa kanisa wa usiku wa leo, ndio wakati wa sita wa kanisa. Kesho usiku tunamalizia nyakati za kanisa; tumechukua mmoja kila usiku, Jumatatu hadi Jumapili. Na usiku wa leo, wakati huu wa kanisa unaitwa Wakati wa Kanisa la Filadelfia. Nayo nyota ama m—mjumbe, malaika—mjumbe kwa wakati huo wa kanisa, tunaamini, kwa uchaji, kwa moyo wetu wote, kuwa ni John Wesley. Wakati huo wa kanisa ulianza mwaka wa 1750 hapo wakati wa kanisa la Kilutheri ulipokwisha, na kudumu hadi mahali fulani katika mwaka wa 1900, yapata 1906 A.D., Wakati wa Kanisa la Kiwesley. Halafu basi, kutoka kwenye huo, ukaja wa Laodikia.

17 Na sasa wakati huo ni wakati wa . . . wakati wa kanisa wa “upendano wa ndugu,” ule wakati mkuu wa “umishenari” na wa “mlango uliofunguliwa.” Nayo zawadi ilikuwa ngu—nguzo, “kufanywa nguzo,” pamoja na ule ufunuo wa majina matatu: jina la Mungu, jina la Mji wa Mungu, na jina jipya la Mungu, ndio ufunuo uliopewa kanisa hili katika wakati huu. Na sasa, kanisa . . . Wakati huu unaanza katika Ufunuo 3:7, hadi kifungu cha 13, na pamoja na kifungu cha 13, Ufunuo 3:7 hadi 13.

18 Sasa, tumekuwa tukipitia haya kidogo usiku, tukirudi nyuma. Nao wakati wa kanisa kwanza, ulikuwa ni Wakati wa Kanisa la Efeso. Mtu yeyote anaweza kusema mara moja ni nani aliyekuwa malaika ama Nuru (mhudumu) wa wakati huo wa kanisa? Paulo. Wakati wa Kanisa la Efeso, mwaka wa 55 A.D. hadi 170. Sababu ya mimi kuuchagua mwaka wa 55, hapo ndipo yeye alipoanza safari yake ya kimishenari, na hapo ndipo alipolianzisha kanisa la Efeso na ninii—na makanisa mbalimbali kule.

19 Vema, wakati wa pili wa kanisa ulikuwa ni Smirna. Mtu yeyote anaweza kukumbuka malaika wa wakati huo wa kanisa alikuwa ni nani, yeyote humu darasani? Ireneo, ni kweli. Vema, ulikuwa ni mwaka wa 170 hadi 312.

20 Wakati wa tatu wa kanisa ulikuwa ni Wakati wa Kanisa la Pergamo. Mtu yeyote anaweza kukumbuka, humu darasani, mtakatifu wa wakati huo wa kanisa alikuwa ni nani? Mtakatifu Martin, ni kweli. Kutoka mwaka wa 312 hadi 606.

21 Halafu basi wakati mwingine wa kanisa ulikuwa Thiatira. Mtu yeyote anaweza kumkumbuka yule mtakatifu na mjumbe, malaika wa wakati huo? Columba, ni kweli. Na hiyo ni mwaka wa 606 hadi '515.

22 Uliofuata ulikuwa ni Wakati wa Kanisa la Sardi, ambao ulikuwa jana usiku. Na mtu yeyote. . .hakika, mnajua malaika wa kanisa hilo alikuwa ni nani. Mnakumbuka? Martin Luther. Halafu wake ulikuwa ni mwaka wa 1520 hadi 1750.

23 Basi usiku wa leo tuko kwenye Wakati wa Kanisa la Filadelfia; ambao ni John Wesley, mjumbe wa siku hiyo. Tangu mwaka wa 1750 hadi 1906 A.D., nao ni wakati wa “upendano wa ndugu.”

24 Sasa, tunaona ya kwamba kila moja ya makanisa haya, nyakati za kanisa, ulionyesha tabia ya kanisa hilo. Zi—zilielezea kile kanisa hilo lilichokuwa pamoja na tabia za hilo kanisa, tabia, hasa, za hilo kanisa.

25 Sasa, jana usiku ilikuwa ni Martin Luther. Mimi. . .katika haya, mimi ni. . .Sababu ya mimi kupata hili nao hawa wavulana wanayaweka kwenye kanda. . .Ninasoma siku nzima. Nanyi mnasema, “Ati siku nzima juu ya ile historia ndogo unayotoa hapa?” La. Mambo muhimu ya kihistoria yataingizwa kwenye kile kitabu, mnaona. Hii hapa, nina. . .sababu ya kufika hapa, ni kuyavuta mambo haya kwa uvuvio kutoka mbele zenu enyi watu, ambapo tunakusanyika pamoja kupata sehemu yake ya uvuvio. Historia, ninaweza kuisoma hiyo kutoka kwenye kitabu. Lakini hapa ndipo ninatarajia uvuvio, kisha tunauchukua kutoka kwenye kanda. Halafu tuna—tuna. . . Katika hicho kitabu, basi, tutakuwa na data yake ya kihistoria na pia ule uvuvio wa Roho Mtakatifu umetupatia wakati tukiwa pamoja hapa, mahali hapa pa mbinguni katika Kristo Yesu. Nami ninaamini inapaswa kukifanya kuwa ni mafafanuzi mazuri sana ya nyakati hizi za kanisa. Basi Bwana na atujalie baraka Zake kwake.

26 Sasa, ninii. . .Jana usiku, wakati wa kanisa, ninii. . .ukiwa ni Wakati wa Kanisa la *Sardi*, kweli katika Kiyunani uliitwa, “aliyeponyoka,” bali ninaamini katika tafsiri ya Kiingereza ni “kufa.” Sasa, lilikuwa ni kanisa “lililokufa” na pia “lililoponyoka” kwa sababu lilikuwa ni kanisa ambalo lilikuwa limekufa chini ya utawala wa kipapa katika mwaka wa yapata

1500, ama 1520, wa—wa ule utawala mkuu wa kipapa ambao tunaita Nyakati za Giza; ambapo Ukristo ulikuwa katika kiwango cha chini sana uliowahi kuwa ama utakavyopata kuwa, hata katika Wakati wa Kanisa la Laodikia.

²⁷ Sasa, kuna jambo moja la kuvutia hata hivyo, endelea kukumbuka niani mwako ya kwamba nyakati hizi za kanisa huanza, na chochote kilicho kwenye wakati huo mmoja wa kanisa kinaenda kote kote kupitia kwenye kila wakati wa kanisa, na kila mmoja wa hizo nyakati za kanisa unaingiliana na huo mwingine. Ukisoma historia kwa makini pamoja na hicho kitabu, utaona.

²⁸ Ni kama mpandano namna *hii*, mmoja ukiwa juu ya mwingine. Ndipo wakati mmoja wa kanisa unaondoka, naye malaika anayekuja katikati ya hapo ataliita kanisa hilo lirudi kwenye imani ambayo liliipoteza wakati mmoja. Sikuzote imekuwa hivyo.

²⁹ Angalia kwenye Yuda, kitabu cha mwisho katika Biblia, mnaona, mpaka unapofikia Ufunuo pale. Yuda alisema, “Niliwaandikia—niliwaandikia ya kwamba mwishindanie Imani waliyokabidhiwa watakatifu mara moja.” Ule mpandano, kati ya mitume na kule kuja kwa Ufunuo, kwa kuwa karibu mitume wote walikuwa wamekufa wakati huo. Mnaona, walikuwa wameondoka. Mmoja alikuwa hai wakati huo, huyo alikuwa ni Yohana Mtakatifu, yule mtawa, ambaye ni mfunuzi ama mwandishi aliyeupata ule Ufunuo kutoka kwa malaika wa Bwana kuandika Kitabu cha Ufunuo.

³⁰ Sasa, mnaona, zinapandana. Kwa hiyo sasa nyinyi... Nadhani mmeona hilo na mmelichukua, wakati tukishuka huku, jinsi nimekuwa nikilitaja. Jinsi ambavyo hata hapa katika wakati wa—wa *Sardi*, huo ulikuwa wakati wa ndoa. Kwa kweli, kanisa kweli halikutokea kikamilifu mpaka Thiatira, bali likaolewa katika *Sardi*. Nayo *Sardi* inamaanisha “kuwa katika ndo—ndoa.”

³¹ Sasa—sasa kama ukiangalia liliolewa *hapa*, kisha likapandana na ule wakati *pale*. Nanyi mnaona Luther, jana usiku, alitokea na jina “lililokufa,” jina la wafu, halafu “aliyeponyoka.” Mnaona, lilikuwa na kanisa lililokufa kutoka *hapa* nyuma, na kule kuponyoka kwa wale masalia wachache waliotolewa katika wakati huo *hapa*.

³² Na usiku wa leo tunapomalizia wakati wa Filadelfia, ni kuingiza mwanzoni mwa wakati wa Laodikia.

³³ Ndipo kesho usiku wakati utakapoondoka kwenye... mwishoni tu, mnaona, malaika anajitokeza moja kwa moja wakati wa mwisho (na kwenye wakati tu wa mwisho) kulikemea kanisa kwa ajili ya kupoteza upendo wake wa kwanza na jinsi lilivyomwacha Mungu kama walivyofanya kote kupitia kule, zile nyakati. Na, kwenye wakati huo Unyakuo unakuja kulipeleka

Kanisa Nyumbani, Kanisa linapaa juu kwenye wakati tu wa huu Ujumbe. Na kwa hiyo tuna—tunaukaribia wakati huo sasa. Mililipata hilo? Vema. Mnaona? Vema. Mnaona, wakati ule ule tu ma—malaika wa kanisa (mjumbe wa wakati huo) anapokuja kuwakemea kwa ajili ya kuupoteza upendo wao wa kwanza, kuwaleta . . . kujaribu kuwarudisha.

³⁴ Jambo lile lile huyu mjumbe analofanya usiku wa leo, malaika-mjumbe anarudi kuwakemea (kila wakati namna hiyo) kwa ajili ya yale waliyokuwa wamefanya. Kwa hiyo hilo linafanya mpandano katika kila moja ya hizo nyakati za kanisa, zinaingiana tu mmoja kwa mwingine namna hiyo. Sawasawa na kupanda kipandio, vinawekwa katika mpandano namna *hiyo*, vikipanda juu.

³⁵ Sasa nina kipande kidogo tu cha historia hapa juu ya huyu mjumbe kwa ajili ya usiku wa leo, ya John Wesley. John Wesley alikuwa nyota ya wakati huo. Naye alizaliwa tarehe 17 Juni, mwaka wa 1703, Nyumba ya Paroko huko Epworth, Uingereza. Alikuwa mtoto wa kumi na tano kati ya watoto kumi na tisa. John na Susanna Wesley, baba na mama. Baba, mhubiri; mama, mtakatifu aliyewekwa wakfu; ingawa alikuwa na watoto kumi na tisa wa kulea, yeye alipata wakati mwingi kupitia siku yake yenye shughuli nyingi kuwafundisha watoto wake masomo ya Biblia na hadithi za Biblia pamoja na kuwaombea. Hilo ndilo lililowafanya hao wavulana kile walichokuwa. Yule mwandishi mkuu wa nyimbo, Charles, ndugu yake, ambaye aliupa ulimwengu baadhi ya nyimbo zinazotia moyo sana tulizopata kuwa nazo.

³⁶ John, mwenzake George Whitefield. John—John Wesley na George—George Whitefield kweli alikuwa ni mwanzilishi wa kwanza wa Methodisti hii . . . ama utakaso.

³⁷ John aliamka mapema kila alfajiri; kwa muda wa miaka sitini aliamka kila siku saa kumi alfajiri. Hilo ndilo jambo moja kanisa limepungukiwa. Aliamka kila siku saa kumi usiku, kisha akahubiri saa kumi na moja alfajiri kwa miaka hamsini mfululizo. Na wakati mwingine alihubiri kutoka mara mbili hadi mara nne kwa siku. Inasemekana na watu wa Uingereza, ya kwamba, “Yeye alisafiri kwa farasi umbali wa maili za Kiingereza elfu nne mia tano kila mwaka, kuihubiri Injili.” Maili elfu nne mia tano kwenye . . . Hizo ni maili za Kiingereza, mwajua, ni ndefu kuliko zetu; kuihubiri Injili.

³⁸ Vitabu vingi vyake . . . viliandikwa vya kumkashifu katika siku zake, vikimkashifu, vikimdhihaki. Bali vimesahaulika muda mrefu sasa, na waandishi wavyo pia. Huwezi kufanya chochote dhidi ya mtoto wa Mungu na kupita nacho, unaninii tu—unapigana tu na hewa. Mungu atawafanikisha moja kwa moja, kwa vyovyote vile.

³⁹ Aliitwa Mmethodisti kwa sababu ya utaratibu wake wa kufanya mambo. Inasemwa, “Maishani mwake,” kwamba, “alihubiri zaidi ya mahubiri elfu arobaini.” Wazia hilo: mahubiri elfu arobaini. Muda kidogo baada ya kuondoka kwake katika mwaka wa 1791, dhehebu la Methodisti liliimarika ulimwenguni na kuanzisha kanisa la Kimethodisti. Halafu, bila shaka, Asbury na wengine wengi walikuwako wakati huo.

⁴⁰ Sasa, kama tukiangalia, salamu kwa kanisa hili; kwa kuwa tutaanzia sasa kwenye kifungu cha 7, mjumbe wa Filadelfia. Kanisa la kweli katika—Kanisa la kweli katika kanisa linaloungama. Lilikuwa Kanisa la kweli katika maungamo.

...kwa malaika wa kanisa lililoko Filadelfia andika;...

⁴¹ Nimevutia usikivu wenu kwenye kule kupandana, kila moja, sasa. Sasa, mtapata hapa, malaika...kama mtaangalia jinsi alivyuingiza wakati wa...Wakati wa Kimethodisti ukipanda, nao utaingia kidogo katika Filadelfia...ama kwenye Laodikia, wakati wa Kipentekoste. Halafu, kesho usiku, mjumbe wa Kipentekoste anarudi kuwakemea hawa kwa sababu ya kuanguka, kama tu vile wakati huu ulivyowakemea kwa kuanguka hapa katika Sardi (katika wakati wa Kilutheri), kule kupandana.

⁴² Upendano wa ndugu. Ulikuwa ni wakati mkuu wa wamishenari na misheni. Ulimwengu haujawahi kuona wakati, hata unaingia kwenye wakati wetu sasa, ambapo, wakati ulimwengu ulipata kuona wakati kama huo wa wamishenari kila mahali. Katika ninii ya mwisho...Loo, ningesema miaka mia moja na hamsini iliyopita, umekuwa ni mmoja wa nyakati za ajabu sana za historia ya ulimwengu huku wamishenari wakiingia katika sehemu zote za ulimwengu pamoja na Injili. Umekuwa...

⁴³ Kwa uhalisi—kwa uhalisi, wakienda tu, wakiutuma ujumbe wa Injili kwa karatasi na vitini na vitabu na kadhalika, Injili imekwisha kwenda kwa kila taifa chini ya mbingu kitambo, zamani sana. Kwa hiyo, mnaona, hiyo inathibitisha ya kwamba hilo halikuwa lile Yesu alikuwa akinena habari zake. Kamwe hakusema, “Enendeni ulimwenguni kote mkajenge shule za Biblia.” Wala hakusema, “Enendeni ulimwenguni kote mkasambaze vitabu.”

⁴⁴ Mambo hayo ni sawa, lakini agizo Lake kwa Kanisa lilikuwa, “Enendeni ulimwenguni kote mkaihubiri Injili.” Na Injili kwa jumla si Neno, bali ni kulifanya hilo Neno lipate Uhai. Mnaona? Kwa sababu Yesu alisema, mara, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Mnajua, Marko 16, ninii Yake ya mwisho—misheni Yake ya mwisho kwa Kanisa ilikuwa, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Agizo Lake la kwanza kwa Kanisa, katika Mathayo mlango wa 10, lilikuwa, “Mwaponye

wagonjwa, mkawafufue wafu, mkawatoe pepo; mmepewa bure, toeni bure.” Nao Ujumbe Wake wa mwisho kwa Kanisa ulikuwa, “Enendeni ulimwenguni kote mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe. Aaminiye na kubatizwa ataokolewa, asiyeamini atahukumiwa, na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.”

⁴⁵ Si ni ajabu kwamba wengi hukatilia mbali sehemu hiyo hapo? “*Na*” ni kiunganishi kinachoifunganisha sentensi yako pamoja, mnaona. Sasa, Yeye alisema, (Wahudumu wengi watasema, “Enendeni mkaihubiri Injili.”) “Aaminiye na kubatizwa ataokolewa, *na* yeye asiyeamini atahukumiwa, *na* ishara hizi zitafuatana na hao. Zitafuatana nao; *hao* waaminio. Katika Jina Langu watatoa pepo; watanena kwa lugha mpya. Wakishika nyoka, ama kunywa kitu cha kufisha, hakitawadhuru; wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya.” Ishara za Mungu aliye hai zikitenda kazi miongoni mwa watu. Loo! Umbali gani sasa? Ulimwenguni kote. Mnalipata? Ulimwenguni kote.

⁴⁶ Kwa hiyo basi wakati ninaposema ya kwamba Ujumbe wa kipentekoste... (Sio dhehebu la Kipentekoste sasa.) Ujumbe wa kipentekoste ndio Ujumbe pekee wa kweli kutoka kwa Mungu. Sasa angalieni, Marko 16, kama mnaisoma pale. Vema, papa hapa Yesu aliliagiza Kanisa Lake, “Enendeni ulimwenguni kote; mkaihubiri Injili; ishara hizi: kunena kwa lugha, kuwaponya wagonjwa, kufanya miujiza...” Zitadumu mpaka lini? “Ulimwenguni kote.” Wa—wangapi? “Kwa kila kiumbe.” Hiyo ni kote kote hata mwisho hapa, “Hata ukamilifu wa dahari.” Vema. Ati ishara hizi zitafuatana na kanisa *hili* pekee? “Hao waaminio, ulimwenguni kote. Ulimwenguni kote, kwa kila kiumbe, ishara hizi zitafuatana nao.” Sio *hawa*, “hao” waaminio. Kwa hiyo ni Kanisa la kipentekoste. Mnaona?

⁴⁷ Sasa, tumeuchukua wakati huu, papa hapa mahali tulipo usiku wa leo juu ya Filadelfia, *F-i-l*, Wakati wa Kanisa la Filadelfia. Katika wakati huo pale, uinjilisti na umishenari umefanywa, kote ulimwenguni kwa vitabu.

⁴⁸ Yesu alisema, “Wakati Injili hii itakapohubiriwa—*Injili* hii itakapohubiriwa ulimwenguni kote kwa ushuhuda Wangu, ndipo mwisho utakapokuja.” Vema, basi, kama hilo ndilo alilokuwa akinena habari zake, kusambaza vitabu, kuwatuma wamishenari pamoja na kusoma, kuandika, hisabati, na kusambaza vitini na kuwafanya watu wapeane mikono na kuamini kwamba kuna Mungu, ikiwa yalikuwa ni hayo tu, basi amechelewa sana katika kuja Kwake. Uh-huh. Kwa hiyo inaonyesha ya kwamba Injili... Paulo alisema, “Injili haikuja kwa neno pekee, bali kwa nguvu na madhihirisho ya Roho Mtakatifu.”

⁴⁹ Ndipo Yesu aliposema, “Enendeni ulimwenguni kote mkaihubiri Injili,” Yeye alisema, “Enendeni ulimwenguni kote

mkadhahirishe!” Loo, ninapenda hilo. “Mkazidhihirishe nguvu za Injili.” Mkilichukua Neno, yale lisemayo, na kuwaonyesha watu kile lisemacho kisha mlidhihirishe kwao. Loo, njia ndiyo hiyo. Hilo linalithibitisha.

⁵⁰ Loo, wakati yule Morris Reidhead mashuhuri, akisimama pale chumbani mwangu siku ile, Rais wa Misheni za Sudan, zilizo kubwa kuliko zote ulimwenguni; hapo aliposema, “Ndugu Branham, wewe ukiwa ni Mbaptisti, inakupasa kujua yaliyo Kweli.”

Nikasema, “Biblia ni Kweli.”

Kisha akasema, “Vema...” Akasema, “Kwani hawa Wapentekoste wana nini?”

Nikasema, “Roho Mtakatifu.” Mnaona?

Na kwa hiyo yeye akasema, “Loo, nimewaona wakivunja fenicha na kurusha vitu kwa mateke.”

⁵¹ Nikasema “Naam! Jambo pekee lililoko, ni kwamba ninyi watu mnajizuia na kujitenga nao.” Wana mvuke mwingi, wangeweza kulifanya gurudumu libingirike na kufanya jambo fulani, bali wanautoa wote kutoka kwenye filimbi, mnaona. Nikasema, “Kama wengeuweka tu hapa chini, wangukuwa na ishara, maajabu, na miujiza, na kila kitu. Lakini hawajui la kufanya nao, hauna budi kwenda mahali fulani, kwa hiyo wanainii tu—wanautumia kwa kupigia makelele, na kuutoa wote.”

⁵² Hmm, afadhali niwe nikiutoa wote, kuliko kuushikilia wala nisiwe na mvuke wowote wa kutoa. Nanyi je? Kama vile yule mzee alivyozoea kusema, “Afadhali niogope maskini ninii wa kigeni...afadhali niwe na moto mdogo wa kigeni kuliko kutokuwa na moto hata kidogo.”

⁵³ Shida yake siku hizi, tunajaribu *kuchora* moto, kusema, “Mwajua, huko nyuma kabisa katika siku za Pentekoste, walifanya jambo *hili*.” Sasa, inafaa nini kumwonyesha mtu anayeganda kwa baridi (hiyo ni kufa kwa baridi) moto wa kuchorwa? Hautamsaidia hata kidogo. La. Huna budi...Hana budi kupata moto yeye mwenyewe. Na ikiwa kuna nguvu za Mungu zilizowafanya Wapentekoste wamfanyie Bwana kazi, na kufanya kazi na ishara walizofanya; kama *hutaichora* tu hiyo picha, bali uwalettee hiyo picha katika uhalisi, watapata tukio lile lile, wokovu ule ule, wautie muhuri ushuhuda wao jinsi *hao* walivyofanya. Mnaona? Bali huna budi kuupeleka kwao. Inakubidi si kuuweka huko nyuma kwenye kizazi kingine, bali kuuleta hapa juu.

⁵⁴ Sasa tunaona ya kwamba wakati huu wa upendano wa ndugu ulikuwa ni wakati mkuu wa umishenari. Yesu alisema, “Ulimwenguni mwote, na kwa kila kiumbe, *na* ishara hizi zitafuata.”

55 Sasa, tulivyoshuka kupitia kwa historia na kupitia kwenye Biblia, nataka kuwaulizeni, hivi si kila usiku . . ? Tunasoma katika Biblia hapa yale Yesu aliyomwambia Yohana yangetukia, na papa hapa tukaichukua historia na kuthibitisha yalitukia. Vivyo hivyo hasa. Na hiyo ndiyo sababu nilikuwa na wakati mgumu hivi nikiwatafuta hawa—hawa watu nione mahali alipokuwa mtumishi huyo wa Mungu ambaye aliubeba ujumbe huu moja kwa moja, bali alikuwako. Alikuwako, kama tu vile Biblia ilivyosema, akauweka Ujumbe kama tu tangu mwanzo, hakucheza Nao.

56 Halafu tukaona karibu uondolewe kabisa, Naye akauita wakati uo huo “wakati uliokufa,” wenye giza, kadhalika. Ndipo ikatokea nuru kidogo tu, kisha nguvu nyingi zaidi, kisha ukaingia kwenye pentekoste (ujuzi halisi) tena kwenye wakati wa mwisho kabisa; halafu Bibi-arusi ananyakuliwa, naye huyo akaondoka; ndipo ile Dhiki ikaanza tena, vema, ile Dhiki Kuu inayokuja mbele ya ulimwengu wote.

57 Sasa ule wakati mkuu wa umishenari, upendano wa ndugu, wakati wa misheni. Hebu niwatajije tu baadhi ya watu hodari (halafu ndiyo kwanza niyaandike majina yao hapa chini): John Wesley; George Whitfie- . . Whitefield, alikuwa yapata mwaka wa 1739; Charles G. Finney; Dwight Moody; William Carey, yule mmishenari mashuhuri aliyeenda India mwaka wa 1773; David Livingstone, aliyeenda Afrika Kusini. Mnaona, wote hao, baadhi ya hao watu mashuhuri. Ninii tu . . Nina majina ya wengi wao hapa, watu mashuhuri walioishi katika huo upendano wa ndugu; ambapo, mtu mweusi, mzungu, mtu wa hudhurungi, mtu wa manjano, kuta zote zilivunjwa, nao watu hawa wakaingia kwenye huduma za kimishenari. Upendano wa ndugu, kunyosha mkono kwa mataifa yote kila mahali, na ilifunguliwa kwao ili waweze kwenda. Wakati mwingine wa mlango uliofunguliwa, maana wasingeweza . . Hapo awali wasingaliweza kufanya hivyo, ule upapa na—na upapa wa Rumi na kadhalika uliifunga yote hata wasingaliweza kwenda. Bali katika wakati huo milango ilifunguliwa, maana Yeye alisema ulikuwa ni wakati wa “mlango uliofunguliwa.”

58 Walifungua milango mingi wakati huo: mlango wa Injili, mlango wa huduma za kimishenari, m—m—mlango wa kumrudia Kristo, na kila kitu kilifunguliwa kwenye wakati huo. Nanyi mnaweza kuona walichofanya, ndugu walifanya kazi kubwa kwake.

59 Na kutoka kwa John Wesley, ile nyota baada ya Wakati wa Sardi, baada ya kuja huko akiwaamsha hao waliotoka kwenye Wakati wa Sardi, kwa miaka mia moja na hamsini iliyopita wamishenari mashuhuri (kuliko kipindi chote ama wakati wowote hapo awali) wameishughulikia dunia nzima. Wazia jambo hilo. Kila taifa chini ya mbingu limesikia Neno. Lilikamilika miaka mingi, mingi, mingi iliyopita, mnaona, bali

sio Injili, Neno tu, “Waraka huu bali Roho hutoa Uzima.” Mnaona?

⁶⁰ Wakati niliposimama Afrika Kusini, huko jukwaani siku hiyo, nami nikaona kulikuwako na maelfu mara maelfu walioketi huko nje, Waislamu. Basi nilikutana na mmishenari mmoja wa Kiislamu. Ndipo huyu mmishenari wa Kiislamu akasema, “Loo, kwa ajili ya nafsi hiyo moja ya thamani.” Sasa, mtu huyo alikuwa huko kwa miaka na miaka, naye alikuwa amemleta Mwislamu mmoja kwa Kristo. Kwa maana Uislamu ulitokana na Waamedi na Waajemi, nazo sheria zao hazibadiliki wala kugeuka; wakiisha kuwa Waislamu, ni Waislamu wakati wote.

⁶¹ Kwa hiyo huko walikuwa na nafsi hiyo moja huyu ndugu aliyokuwa akizungunza habari zake, amesimama huko nje uani mwa Pretoria, mji mkuu wa Afrika Kusini. Hiyo ni huko juu kwenye—kwenye jimbo huru, jimbo huru, jimbo la Orange, na huko Transvaal.

⁶² Nasi tukatoka hapo, tukashuka kwenda Capetown na Bloemfontein, na kupitia huko; kisha tukarudi kupitia Grahamstown, East London, kisha tukaingia...tukarudi Johannesburg tena baada ya kuondoka Capetown, tukapanda pwani.

⁶³ Vema, mji wa mwisho tuliingia ulikuwa ni Durban, ambako tuliwakusanya wengi wa wenyeji, kulikuwako na wenyeji mia moja na hamsini ama mia mbili elfu wameketi huko nje, Waislamu, wenyeji, tulikuwa...walikuwa...inachukua majuma kadhaa kuvuka...u—uwanja huo wa mbio za farasi, mkubwa mno kuliko wa Churchill Downs, wa pili kwa ukubwa ulimwenguni; London ina ulio mkubwa kuliko zote, Afrika Kusini, na—na Churchill Downs. Halafu walikuwa na nyua kwa sababu walikuwa na vita vya kikabila, nao polisi (walinzi mia mbili ama mia tatu) wamesimama kule wakisukuma kila moja ya hayo makabila kwenye hizo nyua wasije wakapigana, na kuwanyang’anya silaha, wakiwa na mikuki yao na mikuki mifupi ya kurusha, na kadhalika waliyobeba. Wakiketi sakafuni kule, mmoja akimwalia mwingine kupitia kwa hizo nyua, na vita vya kikabila. Machifu wao juu...wakiwabeba kwa... mtu fulani akiwa na kipepeo kikubwa akiwapepea namna hiyo, na malkia. Malkia wa Rhodesia alishuka akaja na malori ama garimoshi ama mabehewa ishirini na saba yaliyojaa watu kutoka Rhodesia, kuhudhuria mkutano huo. Na ga—garimoshi maalum likatumwa.

⁶⁴ Bwana alikuwa akifanya mambo makuu, maajabu makuu na ishara. Nasi tulikuta nini? Sidney Smith, meya wa Durban; tukitoka nje siku hiyo, nilisema, “Ni nini jamaa yule...kile kibandiko kidogo shingoni mwake, alichojizungushia?” Mtu mweusi, kama vile tungemwita hapa, jamii ya kinegro. Hao ndio

nilikuwa huko kuwahubiria. Na wengi wao hawakuvaa nguo zozote, hata kidogo, wanaume au wanawake. Kwa hiyo basi, yeye alikuwa na sanamu mkononi mwake na alikuwa na kibandiko kidogo shingoni mwake. Nikasema, “Ni kitu gani wao. . . hivyo vibandiko vilivyofungiwa shingoni mwao ni vya nini?”

Akasema, “Hao ni Wakristo.”

Nikasema, “Ati Mkristo? Huku ana sanamu mkononi mwake?”

⁶⁵ Akasema, “Vema, sasa, Ndugu Branham, mimi. . . Yeye ni Msonghai,” kasema, “Ninaweza kuzungumza lugha yake.” Kasema, “Tutaendesha tu twende pale, nawe uzungumze naye, mwite chochote utakacho. Zungumza tu kana kwamba ulikuwa ukitaka kumwuliza maswali yoyote, nitamwuliza kisha nikwambie aliyosema.”

⁶⁶ Kwa hiyo nikasema, “U hali gani, Thomas?” Nilimwita Thomas kwa sababu nilifikiri hilo lilikuwa ni jina zuri lifaalo. Basi nikasema—nikasema, “U—u hali gani, Thomas?” Ndipo akaniangalia. Nami nikasema, “Je, wewe—wewe ni Mkristo?”

“Naam,” a—alikuwa Mkristo.

⁶⁷ Nami nikasema. . . Loo, hakika, hakunijua mimi. Kamwe hakuwa. . . hakuna mmoja wao aliyekuwa ametuona bado. Kwa hiyo nikasema, “Unafanya nini na sanamu hiyo?”

Yeye, “Loo, ba—baba yake aliibeba.” Mnaona, ilikuwa ni—ilikuwa ni mungu. Mnaona?

⁶⁸ Basi nikasema, “Hivi. . . Baba yako aliibeba.” Nikasema, “Vema, hiyo—hiyo siyo sababu ya wewe kuibeba. Wewe ni Mkristo, haikupasi kuibeba.”

⁶⁹ Akasema, “Vema, siku moja simba alimfukuza baba yake, naye akawasha moto kidogo na kukariri ombi ambalo mchawi alimwambia, juu ya sanamu hii, ndipo sanamu hiyo ikamfukuza simba.” Wanyama huwaua wengi wao sana kule. Naye. . .

⁷⁰ Nami nikasema, “Angalia, ha—haikuwa ni ombi ambalo mchawi alikwambia, moto ndio uliomfukuza simba.” Nikasema, “Simba anaogopa moto.” Nami nikasema, “Kama Mkristo, Thomas, hupaswi kuibeba hiyo. Hupaswi kuwa na uhusiano wowote nayo.”

⁷¹ Naye akasema, “Loo, vema,” akasema, “endapo Amoyah. . .” Hizo ni nguvu zisizoonekana, Mungu wetu tusiyemwona. *Amoyah* linamaanisha kitu fulani, “nguvu kama upepo.” Kasema, “E—endapo Amoyah atashindwa, hii haitashindwa.” Kwa hiyo yeye angebeba zote mbili, “Moja isipofanya kazi, hiyo nyingine itafanya.” Sasa, hizo ndizo nguvu za Ukristo. Uh-hum. Naam. Loo, jamani.

⁷² Lakini basi alasiri hiyo, wakati Roho Mtakatifu aliposhuka mkutanoni kwenye uwanja huo wa mbio za farasi na

kuanza kuzifunua siri za moyo, baada ya mimi kuyachukua Maandiko . . .

⁷³ Yapata saa moja, ambapo kweli ilinichukua dakika kumi na tano, maana walikuwa na wafasiri kumi na watano mbalimbali wa kupitia. Kwa hiyo ni—ningesema kitu kama, “Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu”; na *huyu* aseme, “ah, baa, baa, baa, baa”; na *huyu* afanye, “gloo, gloo, gloo, gloo”; *halafu*, “um, um, um,” namna hiyo; yote yalimaanisha “Yesu Kristo Mwana wa Mungu”; wakalimani. Nami ingenibidi kuandika niliyosema mara ya mwisho, nisingejua mahali nilipokuwa, kisha ningoje mpaka wamalize.

⁷⁴ Ndipo zamu iliponirudia, nikasema, “Sasa, wamishenari waliwaambia juu ya Yesu ambaye alikuja kuwaokoa.” Ungewaona wakiangaliana, mwajua, makabila mbalimbali, kote kote juu na chini namna hiyo. Nikasema, “Wamishenari waliwaambia hivyo. Lakini huyo mmishenari . . . Katika kusoma Kitabu hiki, mliona pale ambapo Yeye alikuwa ni Mponyaji mkuu na ikasema ya kwamba angeishi kote katika wakati ndani ya watu hata atakapokuja tena? ‘Kazi nizifanyazo ninyi nanyi mtazifanya.’ Ninyi ambao mmepata kumkubali Kristo kama Mwokozi wenu, mkiwa na hivyo vibandiko, mnetaka kumwona Yesu akirudi hapa leo na kutembea katikati ya watu na kufanya jambo lile lile alilofanya wakati alipokuwa hapa duniani?”

⁷⁵ Loo, wote, “Hakika!” Walitaka kuona hilo, mnaona. Walitaka hilo.

⁷⁶ Nikasema, “Basi kama Yeye atafanya hivyo, atutumie hapa kufanya jambo lile lile alilofanya alipokuwa hapa duniani, mgeliimini Neno Lake?”

“Loo, hakika!” Mnaona, Waislamu wakiketi huko nje.

⁷⁷ Wa kwanza . . . mtu wa pili jukwaani alikuwa ni mwanamke Mwislamu. Roho Mtakatifu akizungumza, nikamwambia mwanamke huyo mimi mwenyewe, nikasema, “Sasa, unajua mimi sikujui, hata siwezi kuzungumza lugha yako.” Naye akakubali hilo.

⁷⁸ Alikuwa na doa jekundu papa hapa katikati ya macho yake hapa, ambalo lilimaanisha alikuwa Mwislamu ukoo safi. Kwa hiyo, nikasema, “Vema, sasa, kukuponya wewe, siwezi kukuponya.” Lakini nikasema, “Hivi ulielewa ninii . . . nilichosema alasiri ya leo, ule Ujumbe?”

⁷⁹ Na yeye—yeye akamjibu mkalimani wa Kiislamu kwamba . . . Yeye alikuwa ni Mhindi, kile alichokuwa. Akasema, “Naam, alielewa. Alikuwa amelisoma Agano Jipya.” Loo, naam. Uh-hum.

⁸⁰ Mnaona, wao wanamwamini Mungu, pia. Hao ni uzao wa Ibrahimu, pia. Mnaona? Lakini akasema “alimwamini Mungu,” lakini, “aliamini Muhammad alikuwa nabii Wake.”

Nasi tunaamini Yesu alikuwa Mwanawe. Mnaona? Kwa hiyo akasema, loo, yeye—yeye “alimwamini Mungu.”

⁸¹ Basi nikasema, “Basi kama unajua Agano la Kale na unajua kile Mungu alichokuwa katika watu waliopita, katika nyakati zilizopita, basi Yesu, Yule tunayemwita ‘Kristo,’ alikuwa awe Mungu-Nabii. Yeye. . . walimwua. Unafikiri hawakumwua, maana mlisema yeye alimpanda farasi mweupe akaenda zake. Hivyo ndivyo mnavyofundishwa na kuhani wenu, kwamba, ‘Kamwe hakuuawa, sasa. Naye alikufa kifo cha kawaida mahali pengine, miaka kadhaa baadaye.’”

⁸² Nikasema, “Nyinyi mnaamini hilo. Lakini Yesu huyu, jinsi. . . kulingana na Agano Jipya, Yeye alikufa na akafufuka tena, kisha akamtuma Roho Wake katika Kanisa Lake.” Sasa mnayo, mnaona. Hiyo ndiyo ile changamoto hasa yule Mwislamu aliyompa Billy Graham, mnaona. Jambo lile lile, kanuni ile ile.

⁸³ Nikasema, “Sasa kama. . . Mohammed kamwe hakuwapa ninyi nyote ahadi zozote. Bali Yesu alitupa ahadi, kwamba kazi zile zile alizofanya tungezifanya pia. Sasa, mnakumbuka Yeye alisema katika Yohana Mtakatifu 5:19, ‘Sitendi lolote mpaka Baba anionyeshe.’” Nikasema, “Sasa, kama Yesu atakuja na kunionyesha shida yako ni nini ama kilichokuleta hapa, nikwambie jinsi matokeo yako yalivyokuwa, mambo yako ya nyuma yalivyokuwa, na kile siku zako za usoni zitakuwa, na ikiwa anaweza kukwambia mambo yako ya usoni. . . mambo yako yaliyopita, hakika utaamini ya usoni yatakavyokuwa.”

Akasema, “Hiyo ni kweli.” Mnaona, kupitia mkalimani.

Nami nikasema, “Vema, na afanye hivyo.”

⁸⁴ Na hao wote Waislamu wakisimama tu, wakiangalia, mwajua. Ndipo wakati Roho Mtakatifu aliposema, “Mumeo, mfupi, mnene, mwenye masharubu meusi. Ulikuwa kwa daktari, yapata siku tatu zilizopita.” Nikasema, “Una watoto wawili. Alikufanyia uchunguzi wa kike, akasema, ‘Ulikuwa na uvimbe kwenye tumbo la uzazi.’”

Akaangalia chini, akainamisha kichwa chake, kasema, “Hiyo ni kweli.”

⁸⁵ Nami nikasema, “Sasa, kama ukisoma Agano Jipya, hivyo ni kama vile Yesu Kristo Yule aliyemwambia yule mwanamke kisimani?”

“Hiyo ni kweli.”

⁸⁶ Nami nikasema, “Vema, kwa nini ukanijia mimi kama Mkristo? Kwa nini hukumwendea nabii wako wa Kiislamu?”

Akasema, “Nafikiri unaweza kunisaidia.”

⁸⁷ Ndipo nikasema, “Siwezi kukusaidia. Lakini kama utamkubali huyu Yesu Ambaye yuko hapa sasa, Ambaye

anayajua maisha yako na anajua yote kukuhusu, Yeye atakusaidia.”

Akasema, “Namkubali Yesu kama Mwokozi wangu.”

⁸⁸ Hilo lilitosha. Hilo lilikuwa ndilo. Waislamu elfu kumi wakamjia Kristo alasiri hiyo. Mnaona? Yapata miaka thelathini kwenye huduma ya kimishenari, na ilimgeuza mmoja kwa vitabu; ambapo, katika dakika tano, elfu kumi walikuja kwa kudhihirishwa kwa Injili.

⁸⁹ Mungu kamwe hakutwambia tujenge makanisa, kamwe hakutwambia tujenge shule. Hayo ni sawa. Hospitali na kadhalika, Mungu anajua tunazihitaji, ni mpango Wake; bali agizo la Kanisa ni “Kuihubiri Injili!” Lakini tunasambaza vitini, vitabu kutoka Asbury, maskini mahali hapa pazuri hapa juu ambapo. . . Mungu awabariki hao watu, maskini chuo hicho cha Kimethodisti hapa juu Wilmore, Kentucky, ni moja ya mahali pazuri sana, pa kiroho, sehemu ndogondogo ulimwenguni, nadhani, wakati huu. Hao ni watu wazuri.

⁹⁰ Nami nilikuwa nikishuka kutoka kwa. . . nasahau. . . Ilikuwa ni Rhodesia, bali sijui jina la mji huo. Billy, waweza kuukumbuka? [Billy Paul anasema, “Salisbury.”—Mh.] Salisbury, hiyo ni kweli, New Salisbury. (Yeye ndiye kumbukumbu yangu.) New Salisbury, Rhodesia. Nasi tulikuwa tukishuka kutoka Rhodesia ndipo nikaona pasi ya Kimarekani tulipokuwa tukipanda ndege, mvulana mmoja na wasichana watatu. Nami nikasema. . . nikawaendea, nikasema, “Aloo hapo.” Nikasema, “Ninaona mna pasi ya Marekani.”

Akasema, “Unazungumza Kiingereza.”

Nikasema, “Naam,” nikasema, “Mimi—mimi ni Mmarekani.”

Akasema, “Vema, hilo ni sawa.”

Nikasema, “Mnasafiri.”

Akasema, “La, sisi ni wamishenari.”

Nikasema, “Loo, ni vema jinsi gani!” Nikasema, “Hakika nina furaha kukutana nanyi.” Kisha nikasema, “Mmetoka wapi? Kanisa gani, ama ninyi mko pamoja na dhehebu fulani, ama mko huru tu?”

Akasema, “La, sisi ni Wamethodisti. Tumetoka Wilmore, Kentucky.”

Nikasema, “Karibu ni jirani yangu, huko nyumbani.” Nikasema. . .

Akasema, “Haimkini wewe ni yule Ndugu Branham hapa juu?”

⁹¹ Nikasema, “Naam, bwana. Hiyo ni kweli.” Na hilo—hilo lilimponya papo hapo. Mnaona. Asingesema lingine. Nami ni—niliona msimamo aliouchukua, nikawaangalia hao wasichana,

wakaangaliana namna *hiyo*. Nikasema, “Hebu kidogo, mwanangu.” Hakuwa kitu ila mvulana. Nami nikasema... na hao wasichana. Ndipo nikasema, “Ningetaka kuzungumza nanyi nyote kwa dakika moja tu juu ya kanuni za Wakristo, ndivyo tulivyo sisi sote, nasi tupo hapa kwa ajili ya huduma iyo hiyo kuu. Ninataka kuwauliza ninyi wasichana watatu na wewe kijana mwanamume, ‘Mwaweza katika Jina la Bwana Yesu...’ Mlisema mmekuwa hapa miaka miwili. ‘Mwaweza kuweka kidole chenu juu ya nafsi moja ambayo mmeileta kwa Bwana? Nafsi moja?’” Hawangeweza kufanya hivyo. Si hata nafsi moja.

⁹² Nikasema, “Sitaki kuwaudhi, hata kidogo.” Nikasema, “Ninathamini yale mnayofanya, bali ninyi wasichana mnapaswa kuwa nyumbani mkiwasaidia mama zenu kuosha vyombo. Hiyo ni kweli kabisa. Hamna shughuli yoyote hapa. Hiyo ni kweli kabisa.”

⁹³ Wala hakuna aliye na shughuli kwenda hudumani isipokuwa wamempokea Roho Mtakatifu na kuhubiri nguvu za madhihirisho, maana ndicho kitu pekee kitakacho—kitakachowatikisa watu hao. Basi angalieni maasi mliyo nayo sasa na kila kitu, ni kwa sababu kwamba hawajahubiriwa Injili ya kweli. Wamepewa kwa mfano wa neno. Vema, mnaona kile hilo lilicho? Huo ni mwendeleo wa—wa “walioponyoka” wa wakati wa Luther, ambapo uliwapatia walimwengu mitambo huru ya kuchapishia, hiyo ni kweli, ama Biblia ya bure.

⁹⁴ Sasa, sasa wakati, ule wakati mkuu. Sasa, hebu tuanze sasa, ninaamini tuko kwenye... Hizo zilikuwa salamu, kifungu cha 7. Kupitia...

...kwa... *Filadelfia andika; Haya ndiyo asemayo yeye aliye mtakatifu, aliye wa kweli, aliye na funguo za Daudi, yeye mwenye kufungua, wala hapana afungaye; naye afunga, wala hapana afunguaye.*

⁹⁵ Tamshi kwelikweli! Sivyo? Ni—nitarudi kwenye hilo katika dakika moja, maana li—linatumika mbele kidogo katika Maandiko hapa.

Nayajua matendo yako: Tazama, nimeweka mbele yako mlango uliofunguliwa, ambao hapana awezaye kuufunga: kwa kuwa unazo nguvu kidogo, nawe umelitunza neno langu, wala hukulikana jina langu.

⁹⁶ Sasa, sasa angalia wa—wakati unaokuja sasa, baada ya ule wakati mkuu wa kimishenari kuenea kote katika mataifa, wa upendano wa ndugu, kupeleka walichokuwa nacho. Sina neno dhidi yao, juu ya vitabu na kadhalika, katika mahali mbalimbali, ulimwenguni. Sasa, kanisa la kimadhehebu lilikuwa limerejea kwenye matendo ya kielimu tena. Mnaona, limerudi.

⁹⁷ Baada ya lile dhehebu kuu kuundwa, Yesu aliweka “mlango uliofunguliwa.” Baada ya Wakati wa Kiwesley kuja na kanisa

la Methodisti kuimarishwa duniani, likapata mizizi, likakua, likifanyika kanisa kubwa jinsi lilivyo leo, moja ya yaliyo makubwa sana ya, miongoni mwa makanisa ya Kiprotestanti, na wakati huo, jambo lilitukia wakati huo, lilikuwa, Yesu aliweka “mlango uliofunguliwa” kwa ajili ya kanisa kabla hawajaingia kwenye wakati wa Laodikia.

⁹⁸ Sababu ya mimi kusema hili jinsi hii, ili kwamba mpate kuona kile ninachomaanisha kwa mpandano. Mnaona? Ni kutoka kwenye wakati wa kimishenari wa ule mlango. Lakini, mnaona, Yeye alikuwa—Yeye alikuwa amewaambia alikuwa na ufunguo wa Daudi na kadhalika. Lakini hapa alisema alikuwa ameweka mbele ya kanisa sasa; baada ya wakati huo wa kufanya umishenari, na Whitefield, na—na hao wengine wote, na Finney, na Sankey, na Moody na kuendelea (Moody akiwa mmoja wa wale wa mwisho.) kufikia ambapo sasa Yeye anaweka mlango uliofunguliwa mbele ya kanisa. Loo, hapa ndipo inakubidi kuangalia sasa. Ni katikati tu ya wakati wa Fildaelfia na wa Laodikia, mpandano.

⁹⁹ Yesu ndiye Mlango! Sasa, kama mtafungua pamoja nami katika Yohana 10:17. Hebu tuliwekee hili msingi sasa, muwe na hakika ya kwamba. . . Wengi wenu mngeamini. Ndipo mtu fulani angesema, “Vema, kamwe si—sikuninii. . . Yeye alisema hivyo tu.” Ningetaka tu kulisoma. Yohana, mlango wa 10, na kifungu cha 17. Yohana 10:17. Vema, tunasoma Maneno haya. Samahani, Yohana 10:7, si 17.

*Ndipo Yesu akawaambia. . . Amin, amin, nawaambia,
Mimi ndimi mlango wa zizi la kondoo.*

¹⁰⁰ Huko ni kurejea kwenye baraka. Tunaingiaje ndani ya Kristo? Yeye ni nini? Zizi la kondoo. Mara nyingi nilishangaa kuhusu hilo, “Ati nini? Hivi Yeye angeweza kuwa ni Mlango, akiwa ni mwanadamu?” Sasa, huko kwenye—huko kwenye nchi za mashariki kule, nilipata kujua siku moja wakati nilipoona ya kwamba mchungaji, usiku, huwaingiza kondoo wote ndani ya boma, anawaingiza kupitia mlangoni. Ndipo akiwaingiza wote huko ndani, anawahesabu wote aone kama kila mmoja wao yuko ndani. Ndipo anajilaza mlangoni, yeye mwenyewe. Hakuna kitu kinachoweza kuingia penye hao kondoo, wala kondoo yeyote kutoka nje, pasipo kumruka. Kwa hiyo Yesu ni Mlango, mnaona, wa kuingia kwenye zizi la kondoo.

¹⁰¹ Nami nilikuwa nimebebwa na gari dogo aina ya jeep ya Kiingereza, nami nikamwambia jamaa huyo, nikasema, “Wale ni. . .” Wachungaji walikuja kupitia mjini, ndipo filimbi ikapigwa, na kila mtu akafunga breki zao, ndipo nikawazia, “Kwani kuna nini?” Basi ilikuwa ni mchungaji akipitia mjini pamoja na kondoo wake.

¹⁰² Sasa, huko Mashariki, si kama hapa. Wanaweka bidhaa zao zote nje—nje kando ya nyumba sokoni. Na kuna matofaa na

mapeasi, na kila namna ya matunda, na zabibu zimelundikwa juu vizuri sana, zimelundikwa kwenye shubaka kama hili, refu. Na kila mmoja wa wauzaji anasimama pale na kujaribu kukushawishi uingie ununue baadhi ya matunda yake na kadhalika.

¹⁰³ Vema, mchungaji huyu, alianza moja kwa moja kushuka kwenda kwenye barabara hiyo kuu. Nikasema, “Ndugu, hapa ndipo panatokea fujo, nitasimama nione jambo hili.”

¹⁰⁴ Ndipo ndugu aliyekuwa pamoja nami akasema, “Utashangaa, Ndugu Branham. Angalia.” Kila kitu kikasimama. Huyu mchungaji akatembea hapo, bila kujali, kila kondoo akimfuata taratibu kabisa. Akimfuata! Kama alipinduka kidogo namna hii na kugeuka, kila . . . huyo kondoo papo hapo nyuma yake alipinduka, wa pili akamfuata, huyo mwingine akamfuata, moja kwa moja wakapiga hiyo kona.

¹⁰⁵ Loo, hivyo ndivyo tunavyomfuata Mchungaji! Hiyo ni kweli. Akishuka moja kwa moja kupitia katikati ya barabara hiyo kuchukua kitu huko chini kabisa, nao hao kondoo wakimfuata kama tu mbwa. Wangeangalia huko kando na kuona hizo anasa, bali walimfuata mchungaji. Loo, napenda hilo! Mnaona. Nikasema, “Loo, ndugu, laiti ningaliweza tu kuzungumza lugha hii, ningehubiri sasa hivi.” Haya basi. Naam, ha—hakuwa amegeuka kulia wala kushoto, bali alimfuata mchungaji moja kwa moja.

¹⁰⁶ Hivyo ndivyo Kanisa limefanya kote kote, kukaa nyuma ya Mchungaji, Roho Mtakatifu anayetuongoza kwenye Uzima wa Milele; sio kugeuka kwa sababu hili ni kanisa kubwa lenye mapambo, na hili lina madaktari *kadha-wa-kadha* na *kadhalika* namna hiyo, bali dumu kumfuata Mchungaji moja kwa moja. Popote Mchungaji aendapo, kondoo hufuata, “Kondoo Wangu wanaijua Sauti Yangu, na mgeni hawatamfuata.” Hiyo ni kweli. Yeye . . . Mchungaji huyo anajua mguno na kila kitu kinachowafanya hao kondoo wawe na mazoea mazuri.

¹⁰⁷ Ndipo wakati tulipotoka mjini, lilikuwa ni jambo la kushangaza, niliona mbu—mbuga ya malisho pale na watu fulani wamelala kule, nao walikuwa na punda, na ng’ombe, na nguruwe, na kondoo, na mbuzi, na kila kitu huko nje. Ndipo nikasema, “Vema, wale jamaa huko nje ni akina nani?”

Akasema, “Wachungaji.”

Ndipo nikasema, “Kwani mchungaji huwachunga punda?”

Naye akasema, “Ndiyo, bwana.”

Vema, nikasema, “Ni—nilifikiri mchungaji lilimaanisha tu kondoo.”

¹⁰⁸ Akasema, “La. *Mchungaji* ni ‘mlinzi, mlishaji mifugo.’ Na huko nchini mwenu wanawaita ‘kaoboi’ na—na vitu kama hivyo.”

Nikasema, “Loo, sawa, mchungaji ni mlishaji mifugo.”

“Naam.”

“Yeye huyachunga makundi ya mifugo.”

¹⁰⁹ “Hiyo ni kweli.” Yeye akasema, “Jambo la kigeni ni wakati wa usiku, ambapo wewe. . . ni la kushangaza. Wewe ukiwa mhudumu, vema, huenda nikakwambia jambo fulani.” Akasema, “Usiku unapokuja. . . Ni kweli yeye humchunga kila mmoja wao, anawaongoza kote na kuwasaidia na kuona kwamba wanapata mambo mazuri mchana kutwa. Lakini usiku unapoingia. . . nyu—nyumbu wote na punda na nga—ngamia, na wowote alio nao, huachwa kondeni. Lakini yeye huwakusanya kondoo na kuwaingiza kwenye boma.”

¹¹⁰ “Loo,” nikasema, “Bwana, nifanye kondoo, lolote utakalofanya!” Mnaona? Kwa kuwa usiku unapoingia, ninataka kuingia kwenye zizi la kondoo. Niingie kwenye Mlango, nipitie Mlangoni. Yonana 17:7 hapa, ama—ama Yeye alisema, “Mimi ndimi. . .” 10:7, hasa, Yeye alisema, “Mimi ndimi Mlango wa zizi la kondoo. Wote waliopata kunitangulia ni wezi na wanyang’anyi, bali kondoo hawakuwasikia. Mimi ndimi Mlango, mtu akiingia kwa njia ya Mimi, ataokolewa, naye ataingia na kutoka na kupata malisho.”

¹¹¹ “Sasa, nimeweka mbele ya kanisa hili, katikati ya wakati wa Filadelfia na wakati wa Laodikia, mlango uliofunguliwa.” Loo, mnalipata sasa? Nanyi mmevaa vizuri kabisa kofia zenu za kuwazia na zimekaza? Sikilizeni sasa, hili ni zuri. Nawaambia, ni Asali kwenye Mwamba, tunachukua tu vibamba vya madini na kuving’arisha sana. “Mimi ndimi Mlango wa zizi la kondoo!” Huo Mlango uliowekwa ni upi, sasa?

¹¹² Hebu turejee niani mwetu. Na kutoka kwenye huo wakati mkuu wa kimishenari wa Wamethodisti, ambao ulienea nchini kote kwa ujumbe wa utakaso. Luther kwa kuhesabiwa haki. Wesley akaja na ujumbe wa utakaso. Na mwishoni mwa wakati wa Methodisti, mwishoni, wakati ulipoimarika na ukaanza kuwa dhehebu kubwa. Na wakati kanisa lolote. . .

¹¹³ Sasa sikilizeni, hilo ni kali. Bali ninataka mtu fulani anionyeshe popote kwa kuichambua historia. Kanisa lolote ambalo Mungu alipata kuliinua, lilipitia njia ya Kipentekoste pasipo na dhehebu lolote; na mara lilipounda dhehebu, lilikufa wala kamwe halikuinuka tena. Loo, ufuasi uliendelea, bali kamwe hawakupata uamsho. Uamsho wa Luther haukuinuka, na wala uamsho wa Methodisti kamwe haukuinuka, wala uamsho wa Kipentekoste kamwe hautainuka. La, bwana. Waliliundia dhehebu, ambalo Mungu alisema katika nyakati za kanisa, Yeye “anakichukia kitu hicho,” fundisho la Wanikolai.

¹¹⁴ Sasa, kumbukeni, hatuzungumzi dhidi ya mtu yeyote. Watu wazuri wametawanyika. Kondoo wa Mungu wako katika sehemu hizo zote huko nje. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli. Wamethodisti,

Wabaptisti, wowote wale, hao ni watu wa Mungu kama wamezaliwa mara ya pili kwa Roho wa Mungu. Hao ni watu wa Mungu, bali madhehebu yamewakanyagia chini. Na kuchukua barua kutoka Methodisti hadi Baptisti hadi Ukampbeli, na kadhalika, hata wa—wakachakaza barua wakizibeba mahali mahali.

115 Vema, jinsi Mungu alivyosema sasa, mwishoni mwa wakati huo, “Mimi ndimi Mlango wa zizi la kondoo.” Sasa, ni mlango gani uliofunguliwa kuhusu Yesu, katikati tu ya nyakati hizi mbili? Mwaka wa 1906, yapata wakati ule wakati wa Methodisti na—na—na Dwight Moody na hao wengine ulipofikia ukatoweka jukwaani, kulitokea uamsho wa watu kumpokea Roho Mtakatifu, wakinena kwa lugha na kadhalika ulioingia kanisani. Hiyo karibu ni kweli, yapata mwaka wa 1906, mahali fulani pale.

116 Vema, ni kitu gani kilichotukia basi? Baada ya huo kuanza kuingia, muda si muda wajua, waliliundia dhehebu lile Baraza Kuu la kale ambalo liliingia, sasa linaitwa Assemblies of God. Mnaona, kutokana na kanisa hilo lililokuwa na kuingiliana. Basi ni kitu gani kilichotukia? Yeye aliweka mlango uliofunguliwa, “mlango uliofunguliwa.”

117 Sasa hebu tulisome tu sasa, tulishike neno kwa neno jinsi tu Yeye anavyolileta. Mnaona, “Tazama . . .” Hebu tuone:

. . . *hapana awezaye kuufunga; . . .*

. . . *nimeweka mbele yako mlango uliofunguliwa, . . .*

118 Uko upande ule mwingine:

Ninayajua matendo yako: tazama, nimeweka mbele yako mlango uliofunguliwa, wala hapana awezaye kuufunga: . . .

119 “Mlango uliofunguliwa.” Ulikuwa ni nini? Ulikuwa ni ufunuo wa Uungu mkuu wa Yesu Kristo: sio akiwa mtu wa pili wa utatu, bali akiwa Mungu Mwenyewe aliyefanyika mwili na kuishi miongoni mwetu. Nao ufunuo . . .

120 Sasa, kama ukiangalia, kwa dakika moja tu, hebu tusome mbele zaidi kidogo tu:

. . . *kuufunga: . . . unazo nguvu kidogo, . . . wala hukulikana jina langu.*

121 Mara ya kwanza ambapo Jina limetajwa sasa tangu huku nyuma kwenye wakati huu *hapa* nyuma, ulilipoteza Jina lake; naye Luther akatokea akiwa na jina kwamba yu hai, naye alikuwa *amekufa* (Hiyo ni kweli?), “Baba, Mwana, Roho Mtakatifu.” Hili hapa Jina la Yesu linakuja tena, katikati ya nyakati hizi mbili *hapa*. Katikati, “mlango uliofunguliwa.” Sasa, ni ufunuo: kile alichokuwa, Uungu, ufunuo wa Uungu Wake.

122 Sasa, huo ndio alioufungua katika wakati wa kwanza kabisa wa kanisa. Sasa angalia. Kama vile Yohana alivyomwona amesimama, vinara vya taa saba vya dhahabu, naye alikuwa amesimama ameinyosha mikono yake. Huu hapa mnara wa kwanza wa taa, wa pili, wa tatu, wa nne, wa tano, wa sita, wa saba, huku ameinyosha mikono Yake mfano wa msalaba. Alisema, “Mimi ni Alfa na Omega.” Kwa maneno mengine, “Nitakuwa mkuu katika wa kwanza, nitakuwa mkuu katika wa mwisho.” Nuru huchomoza Mashariki na kutua Magharibi. Imekuwa wakati wenye utusitusi, wenye giza, bali “Itakuwa Nuru wakati wa jioni.” Nguvu zile zile za Injili zilizoinuka *hapa* upande mmoja Mashariki, zimeangaza kabisa na sasa kwa upande mwingine Magharibi, “Alfa na Omega, Mimi ni A na Mimi ni Z.” Mikononi Mwake! Mnalipata?

123 Sasa, Yeye alifanya nini katika mlango wa kwanza wa Ufunuo? Alifunua Uungu Wake mkuu kwa kanisa la kwanza, Efeso. Hiyo ni kweli? Vema, sasa angalieni. Kila moja ya makanisa haya likija kupitia hapa, Yeye alijifunua Mwenyewe katika Uungu tu katika hali Yake iliyotukuka; lakini katika huu wa mwisho, Yeye anakuwa Z, amerejea kwenye mwanzo asilia tena. Mnaona, “Wa kwanza na wa mwisho.” Wakati wa kwanza, sasa wakati wa mwisho, kwa kuwa alisema, “Mimi ndimi wa kwanza na wa mwisho.” Na . . .

124 Lakini mnasema, “Vema, hilo lilitukiaje? Ni jamaa yupi aliyechukua hilo?” Ilikuwa ni ufunuo! Wengi wenu hapa ndani mmeupokea, maana ninii Yake yo- . . . Nitasema jambo fulani sasa. Angalieni! Kanisa Lake lote limejengwa juu ya Ufunuo wa Kiungu wa nafsi Yake. Hiyo ni kweli? Kama hamuamini hilo, hebu tufungue Mathayo 16:18, mtaona katika dakika moja tu ya kwamba ufunuo wote umejengwa juu ya nafsi Yake. Kanisa Lake lote limejengwa juu ya funuo za nafsi Yake. Sasa hebu tuanzie hapa kwenye . . . Hebu tuanzie . . . hebu, kwenye yapata kifungu cha 14:

Basi wakasema, Wengine hunena . . . wewe ni Yohana Mbatizaji: . . .

Swa—swali lilikuwa, Yesu alisema:

. . . kwenye pwani ya Kaisaria Filipi, akawauliza wanafunzi wake, akasema, Watu hunena . . . mimi Mwana wa Adamu kuwa ni Nani?

Kifungu cha 13, na hicho ni 16:13 sasa.

Wakasema, . . .

125 Sasa angalieni, hapa ndipo mahali pa kwanza Yesu alipopata kuzungumza juu ya kanisa, na ninii . . . kuendelea mpaka Ufunuo ambapo ndipo pa mwisho.

Na yeye akasema, Wengine hunena...u Yohana Mbatizaji: na wengine, Eliya; wengine, Yemia na wengine...na—na...au mmojawapo wa manabii.

Yeye aka—akawaambia (kundi zima, kundi lote), Lakini nanyi mwaninena kuwa ni nani?

Ndipo Simoni Petro akajibu akasema, Wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai. (Loo, jamani!)

Yesu akajibu akamwambia, Heri wewe, Simoni—Simoni Bar-Yona:... mwili na damu havikukufunulia hili, bali Baba yangu aliye mbinguni.

126 Loo, jamani! “Hukupata hili kutoka kwenye seminari. Hapakuwapo na njia yoyote nyingine uliyopata hili, Simoni, mwana wa Yona; jinsi tu ulivyolipata, ilikuwa ni ufunuo wa kiroho uliofunuliwa kutoka Mbinguni ya kwamba Mimi ndiye.” Yesu alisema, “Msipoamini ya kwamba Mimi ndimi, mtakufa katika dhambi zenu. Mimi Ndimi!”

...nakuambia...wewe,...wewe ndiwe Petro,... juu ya mwamba huu nitalijenga kanisa langu; wala mlango ya kuzimu haiwezi kulishinda.

127 Ni kitu gani? Kiroho! Kiroho! Ukweli wa kiroho! Neno la Bwana!

128 Sasa, tunaona ya kwamba katika ufunuo huu mkuu ambao Mungu alilipa Kanisa hapa, katika siku hizi za mwisho, ya kwamba Mungu alituma na kujifunulia Mwenyewe “Mlango uliofunguliwa” *kati ya* nyakati hizo mbili. Haikuwa katika wa—wakati wa Laodikia, wala haikuwa katika wakati *huu* mwingine (wakati wa Filadelfia), bali ilikuwa katikati (mpandano), maana ninii...Nitalithibitisha katika muda mfupi baadaye tunapoendelea, nanyi mtalipata, mnaona. Tutaliboresha, kwa uhakika sana hata hamwezi kukosa kuliona, ikiwa tu mnataka kuliona, mnaona. Vema.

129 Sasa, ufunuo wa nafsi Yake ndipo amelijenga Kanisa Lake. Ni wangapi wanaojua hilo kwamba ni kweli, sasa? Yeye alilijenga Kanisa Lake juu ya ufunuo wa nafsi Yake. Vema. Sasa Yeye alisema nini? “Hakuna mtu anayeweza kuufunga!”

Nayajua matendo yako: tazama, nimeweka mbele yako mlango uliofunguliwa...

130 Ni nini “mlango uliofunguliwa”? Ufunuo wa Uungu mkuu wa Yesu Kristo! Aliliambia nini Kanisa Lake la kwanza hapa nyuma, nyuma katika wakati *huu*? Alisema, “Mimi Ndimi aliyekuwako, aliyeko, na atakayekuja! Mimi ni wa kwanza na wa mwisho! Mimi ni Mwenyezi!” Alisema hivyo mara tatu mbalimbali, akajifanya Mwenyewe Mungu kwa kanisa hili la kwanza *hapa*; kabla hajaenda kwenye wakati wa mwisho wa kanisa, Yeye alisema, “Nimeweka mbele yako mlango uliofunguliwa.” Kama unataka kuona Ufunuo, Huu hapa,

ambapo Yeye angejenga Kanisa Lake. Na njia pekee ambayo angeweza kulichukua Kanisa Lake, ni kulirejesha kwenye ufunuo wa kile aliche Yeye. Kweli!

¹³¹ Angalieni! Wakati Ibrahimu alipofanya agano, ama Mungu alipofanya agano na Ibrahimu, siku ile aliyosema, “Mambo haya yatakuwaje, kwa kuwa mimi ni mzee? Na mrithi wangu wa pekee ni—ni huyu mtumishi wa Dameski niliye naye hapa, Eliezeri.” Kasema, “Mimi ni mzee, Nawe uliniahidi mtoto. Utafanyaje jambo hili? Litatendwaje?”

¹³² Basi kumbukeni alienda kulala, usingizi mzito ukamjia kama kila mtu afanyavyo; mauti. Ndipo akaona, mbele yake ikatoka ta—tanuru ya moshi; kila mwenye dhambi anapaswa kwenda kuzimuni. Alikuwa amemwua mnyama (ndama), mbuzi jike na kondoo dume, na hua na njiwa. Kamwe hakuwapasua hua na njiwa. Ndipo Nuru hii ndogo nyeupe ikaenda mbele pale, na ikaenda huku na huko kati ya vipande hivi vilivyokatwa vya mnyama, akilithibitisha agano pamoja na Ibrahimu.

¹³³ Sasa, huko Japani, kama ikitokea kuwa na Mjapani hapa, unajua jinsi wanavyofanya agano huko Japani? Wanarushiana chumvi mmoja kwa mwingine. Wanachukua chupa ndogo ya chumvi, na kuketi chini kule, wanazungumza, “Je, utafanya *hivi na hivi*?” “Naam, nitafanya *hivi na hivi*.” Ndipo wanafanya agano na kuchukua chumvi kidogo na kurushiana, maana chumvi huhifadhi, mnaona. Vema. Wanarushiana chumvi, hilo ni agano.

¹³⁴ Huku Marekani, jinsi tunavyofanya agano huku, tunasema, “Vema, utafanya jambo fulani?” “Nitafanya jambo fulani.” Na muda si muda wajua, tunapeana mkono, “Utikise!” Na hilo ni agano.

¹³⁵ Lakini, huko mashariki, jinsi walivyofanya agano, waliandika jambo fulani. Nao wakaandika mkataba, kisha wakamwua mnyama, katika wakati wa Ibrahimu. Wakampasua mnyama huyo na kusimama katikati yake; wakaandika mkataba huu, na kuurarua namna *hii*. Mmoja alichukua kipande kimoja, na huyo mwingine hicho kingine. Ndipo wakala kiapo ya kwamba “miili yao na iwe kama mnyama huyu aliyekufa kama wakishindwa kutimiza mkataba huu.” Na sasa njia pekee ambayo mkataba huu unaweza kuninii. . . Usingeweza kuunakili. Hauna budi kurudi ukiwa ni kitu kile kile, viungane pamoja.

¹³⁶ Sasa, Mungu alikuwa akimwonyesha Ibrahimu Yeye atafanya nini? Ya kwamba atauchukua Uzao wa Ibrahimu, kupitia kwa Isaka hadi Yesu, Naye akampeleka hata Kalvari na hapo akampasua vipande viwili. Akaitoa Roho kutoka Kwake, mbali na mwili, akaufufua huo mwili na kuuweka kwenye mkono wa kuume wa Ukuu huko Juu, kisha akamtuma tena Roho Mtakatifu Kanisani. Hilo ndilo agano la Mungu,

akampasua vipande viwili: sisi tunaye huyo Roho, Yeye anao mwili. Basi wakati vinaporudi pamoja, Roho aliyekuwa ndani yetu anajiunga Naye kama Bibi-arusi. Amina. Hakuna dhehebu lolote lililounganishwa Naye hata kidogo. La, bwana. Ni Kuzaliwa safi, kusikoghoshiwa kwa Roho Mtakatifu. Hivyo tu. Hilo ndilo agano.

¹³⁷ Sasa, sasa tunaona ya kwamba Yeye alisema, “Nimeweka mbele yako mlango uliofunguliwa.” Nami sijali ni mashirika mangapi ya kujibunia yatainuka, ama madhehebu, hata malango ya kuzimu hayawezi kuufunga. Njia moja tu ya kulishinda, jiuje Nalo. Hivyo tu. Huwezi kujiunga Nalo, kwa hiyo huna budi kuzaliwa ndani Yake. Kweli. Kwa hiyo hakuna mtu angaliweza kuukomesha Ujumbe huo wa Uungu mkuu pamoja na ubatizo katika Jina la Yesu Kristo. Malango ya kuzimu hayataweza kuushinda.

¹³⁸ Mnasema, “Unajuaje kwamba ni wa kweli?” Unalingana kabisa na Neno, wala hakuna mtu mwingine anayeweza kusema chochote juu Yake. Kweli kabisa! Ni Neno. Hakuna mahali ambapo mtu yeyote alibatizwa katika jina la “Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu.”

¹³⁹ Huyu Mtakatifu Paulo mashuhuri, malaika wa Efeso, alimwagiza kila mtu ambaye hakuwa amebatizwa, haidhuru umebatizwaje, kama hujapata kubatizwa katika Jina la Yesu Kristo, yeye alikuagiza uje ukabatizwe tena katika Jina la Yesu Kristo. Alisema, “Kama malaika kutoka Mbinguni akiya akifundisha jambo lingine lolote, na alaaniwe.”

¹⁴⁰ Kwa hiyo unaweza kuona kile malaika anayekuja katika siku hizi za mwisho, ni Ujumbe wa aina gani atakaokuwa nao atakapokuja. Huenda tunaelekea kwake. Lakini ninawaambia, atakapokuja, yeye atahubiri ubatizo katika Jina la Yesu Kristo. Kama huamini hilo, njoo huku kesho usiku uache nikuonyeshe kupitia kwa Maandiko. Hakika atahubiri! Na kutahiriwa kwa moyo, na miujiza ya Kiungu, na utenda kazi wa nguvu kama tu vile ilivyokuwa kwenye Siku ya Pentekoste. Baraka zile zile asilia za Pentekoste zitarudi moja kwa moja kwa maskini masalia hao kuwapeleka huko ng'ambo. Mkataba huo utakuwa kama tu ulivyokuwa wakati uliporaruliwa mara ya kwanza. Loo, ninampenda! Nina furaha sana, furaha sana. Si—siwezi kuielezea vizuri vya kutosha. Nina furaha sana kwamba ninaweza kusema mimi ni mmoja wao. Nina furaha sana!

¹⁴¹ Laiti ndugu zangu wote wangalikuwa namna hiyo. Laiti ningaliwafanya ndugu zangu na dada zangu huku nje, marafiki zangu wa thamani huko nje ulimwenguni, kuona jambo hili kuu. Ni—ni—ningeninii, ningekuwa radhi, usiku wa leo, Mungu anajua hili. Nina mvulana mdogo, Joseph, wa kulea; na msichana mdogo, Sarah na Rebekah; na mke mzuri ambaye nachukia kumwacha; bali kama ningalijua ya kwamba ndugu zangu

ko- . . . watu ninaowajua katika ulimwengu huu, wangelikubali Hilo na kuliadini, na wajazwe na Roho Mtakatifu, ningekuwa tayari kuondoka sasa hivi. Hiyo ni kweli kabisa. Mnaona? Loo, laiti ningalinii tu. . . nawe huwezi. . . Kama ukizungumza kwa upole, wanafikiri unajaribu kuwawekelea kitu fulani. Na—na kuna jambo moja tu la kufanya, hilo ni kudumu moja kwa moja na Neno na kulipigilia kabisa. Na hiyo ni kweli kabisa, dumu moja kwa moja Nalo. Loo, jinsi ninavyompenda!

¹⁴² Ufunuo Wake, Uungu Wake mkuu. Kitu gani, Yeye alifanya hivyo? Kamwe siwezi kuliacha, kwa namna fulani. Yeye aliufunua katika kanisa la Efeso. Hiyo ni kweli? Na hapo ilikuwa ni wakati Nuru ilipovunja kwa mara ya kwanza ipate kuangaza, Nuru ya Kikristo. Hiyo ni kweli? Wakati wa Roho Mtakatifu ulianza papa *hapa* Efeso.

¹⁴³ Naye nabii alisema, “Kutakuja siku ambayo si usiku wala mchana, bali wakati wa jioni Nuru hiyo ingerudi tena.” Mnaona? Mnaona. Mnaona, siku hii ya utusitusi, inapitia pale, hizi zote hapa zenye utusitusi (madhehebu na kila kitu); bali katika siku za mwisho upande *huu*, hapa chini kabisa Yeye angeweka mlango uliofunguliwa. Yesu alisema, “Mimi ndimi huo Mlango.”

¹⁴⁴ Je, ulipata kumsikia Yeye akisema, “Mimi ndimi lango. Mimi ndimi njia, Kweli, na Nuru”? Mnaona? Mlipata kumsikia akisema, “Mlango ni mwembamba, na njia imesonga”? Hivi mliwahi kuona jinsi hilo *mwembamba* lilivyowekwa kiherufi? [Kiingereza: Strait—Mf.] S-t-r-a-i-t, maji. *Strait* linamaanisha “maji,” likiwekwa hivyo kiherufi. (S-t-r-a-i-g-h-t, mnaona.) *Strait*, “Maji ndiyo njia. Na hayo maji ndiyo mlango, na njia imesonga.” Maji ni nini? Lango, mlango. Mnaona, kufungua. “Katika Jina la Bwana Yesu ndiyo njia, kupitia kwa maji. Mlango ni mwembamba, njia imesonga, ambayo. . .” Yesu. . . “Maji ndiyo lango, katika Jina la Bwana Yesu, kuingia ndani.”

¹⁴⁵ “Tubuni kila mmoja wenu mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi zenu nanyi mtapokea, wakati mkiangalia Kalvari, kipawa cha Roho Mtakatifu. Kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu na kwa watoto wenu.” (Baadhi yao walisema, “Ni kwa ajili ya mitume tu.”) “Kwa ajili yenu na kwa watoto wenu, na kwa hao walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie.” Hivyo—hivyo tu. “Wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie.” Ahadi hii ni kwa kila mtu, kama utakuja vile vile agizo lisemavyo. Hiyo ni kweli.

¹⁴⁶ Usiseme, “Vema, nitapitia huku kisiri.”

¹⁴⁷ Kuna mtu wakati mmoja aliingia kisiri, mwajua, na akaingilia njia nyingine. Mlijua hilo? Hivi mlipata kusoma mfano wake? Kulikuwa na mtu aliyeingia kisiri na kuingilia njia nyingine. Sasa, huko mashariki, wakati wao—walipokuwa

kwenye karamu ya arusi...Tutalichukua asubuhi: kwenye Karamu ya Arusi, jinsi mtu huyo alivyoingia mle. Tutajaribu, kuchukua hilo asubuhi. Nilikuwa nikitaka kulisema sasa, bali nitaliachilia. Asubuhi: jinsi ambavyo mtu huyo aliingia mahali hapo kutoka kwenye Karamu ya Arusi...ama, kwa ajili ya Karamu ya Arusi.

¹⁴⁸ Vema, “Mlango ni mwembamba, njia imesonga.” Maji ndiyo mlango, kiingilio cha kwenda kwa Bwana Mungu.

¹⁴⁹ “Nimeweka mlango uliofunguliwa. Ninazo funguo. Mimi ndimi pekee ninayeweza kuufungua, Mimi ndimi pekee ninayeweza kuufunua, ninazo funguo.” Hiyo ni kweli. “Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu asipovutwa na Baba Yangu, na wote alionyeza Baba watakuja Kwangu.” Hakuna mtu anayeweza kuokolewa ila kwa Yesu Kristo. Si kupitia kanisa lolote, dhehebu lolote, askofu yeyote, papa, kupitia tu kwa Yesu Kristo. Yeye ana ufunguo, Yeye ndiye pekee anayeweza...Funguo za nini? Daudi, ule Utawala wa Miaka Elfu unaokuja siku za usoni ambapo Yeye ataketi kwenye kiti cha enzi cha Daudi. “Ninazo funguo za Daudi, nitaufungua mlango huu wala hakuna mtu anayeweza kuufunga. Hakuna mtu anayeweza kuufungua ila Mimi, wala hakuna mtu anayeweza kunifungua Mimi.”

¹⁵⁰ Inawezekanaje? Mtu yeyote anawezaje kujua ya kwamba Yeye ndiye Kristo mpaka ajifunue Mwenyewe kwake? Mnaona, Yeye hujifunua Mwenyewe, ana ule ufunguo. Anaweza kuufungua ama kuuachilia. Mnaona? “Ninao ufunguo wa mlango. Mimi ndimi Mlango. Mimi ndimi Njia. Mimi ndimi Kweli. Mimi ndimi Nuru.” Loo! “Mimi ni Alfa. Mimi ni Omega. Mimi ni wa Kwanza na wa Mwisho. Mimi ni Baba. Mimi ni Mwana. Mimi ni Roho Mtakatifu. MIMI NIKO! Sio ‘nilikuwa’ ama ‘nitakuwa.’ MIMI NIKO AMBAYE NIKO, a—aliyesema jambo hilo lote. MIMI NIKO, sio ‘nilikuwa’ wala ‘nitakuwa.’ MIMI NIKO, hilo linamaanisha ‘uwepo ulio hai Milele.’ Mnaona, MIMI NIKO! Daima nilikuwako, daima nitakuwako, Mimi niko sasa kama nilivyokuwa sikuzote na sikuzote nitakuwa.” Mnaona, Yeye—Yeye ni MIMI NIKO tu!

¹⁵¹ Ninazo funguo za Daudi za ufalme, “hakuna mtu anayeweza kuufunga.” Kifungu cha 7 kinathibitisha hilo, vema, kwamba Yeye ana funguo za Daudi, “Hakuna mtu awezaye kufunga!”

¹⁵² Sasa hebu tuone kwamba kitu kinachofuata ni nini, upesi:

... kwa kuwa unazo nguvu kidogo...

¹⁵³ Loo! Kaliambia kundi hili dogo hapa chini, “Unazo nguvu kidogo tu sasa.” Hilo linamaanisha nini? Ni kama tu mtu ambaye amekuwa mfu, kidogo anajitikisa, anaanza kuwa hai, akizinduka kidogo, akifufuka. Umetoka kwenye hizo kanuni za kale zilizokufa na kila kitu, umeanza kupata uhai kidogo, unajitikisa, kidogo unajiamsha. “Unazo nguvu kidogo, bali nimeweka mlango mbele yako sasa.” Mara walipotoka kwenye—

kwenye Ulutheri na upapa, na itikadi hizo zingine zote, na—na Umethodisti na kila kitu, Yeye alisema, “Nimeweka mlango mbele yako, sasa unazo nguvu kidogo, utafanya nini kuhusu hilo? Umewekwa mbele zako, unaweza kuingia ama kutoka, lolote utakalo. Mlango umewekwa mbele zako. Unazo nguvu kidogo, ndio kwanza unaanza kupata Uzima, ndio kwanza unaanza”.

154 Ndivyo ilivyokuwa kwa kanisa la mwanzoni. Tazameni mwishoni mwa wakati wa Laodikia, lilirudi kwenye matendo tena. Sasa, kama mkiangalia hapa, ku—kuonyesha ya kwamba kanisa hili liko katikati ya hizi mbili. Kama ukienda kwenye wakati wa Laodikia, ama Wakati wa Kanisa la Laodikia, “Nayajua matendo yako,” moja kwa moja mwishoni mwa wakati wa Laodikia. Ilikuwa ni nini? “Matendo yako, na kiti alimo Shetani.” Kiti cha Shetani kilikuwa ni nini? Mnaona, lilirudi moja kwa moja katika dhehebu tena.

155 Ninyi Assemblies of God, na Umoja wa Kipentekoste, na Church of God! Loo, hivi hamwoni, ndugu, yale mliyofanya? Mlirudi moja kwa moja kwenye kile kitu ambacho Mungu alichukia, mkavunja udugu. Liangalieni Assemblies of God, baadhi ya watu walio wema sana duniani wako kwenye Assemblies of God. Liangalieni kanisa la United Pentecostal, wazuri tu kama uliowahi kukutana nao maishani mwako. Angalieni kwenye Church of God. Na kwa sababu ya madhehebu hayo, wanazozana na kuzomeana na kuzozana mmoja kwa mwingine, na kuitana “banda la mwewe” na “tundu la panya.” Mbona, ni fedheha!

156 Jambo moja analochukia Mungu ni “kupanda mafarakano miongoni mwa ndugu.” Na hiyo ni kweli. Nao hayo madhehebu ndiyo yafanyayo hivyo, kupanda mafarakano miongoni mwa ndugu. Tunapaswa kuwa tukisimama katika pengo na kusema, “Sisi ni ndugu!”

Hatujagawanyika,
Sisi sote ni mwili mmoja;
Mmoja katika tumaini na fundisho, (Fundisho
la Biblia.)
Mmoja katika upendo.

157 Ninaupenda wimbo huo wa zamani, *Twendeni Askari Wakristo*. Naam, bwana.

158 Mwisho wa Laodikia, walirudi kwenye matendo tena, ama madhehebu ya Kipentekoste yalirudi kwenye dhehebu. Hebu tufungue kifungu cha 15. Nimeandika hapa, “Kifungu cha 15 cha Ufunuo 3.” Na tuone kama hiyo si kweli, sasa. Ufunuo 3, na—na . . . ama hebu tuone, nimeandika hicho vizuri. Ufunuo . . . Loo, la, la, ni—nilikosea, kifungu cha 15. Ni kifungu cha 15 cha mlango uu huu, kinaonyesha jambo lile lile hapa chini. Naam, uh-huh:

Nyajua matendo yako, ya kuwa hu baridi wala hu moto: . . .

¹⁵⁹ “Nyajua matendo yako.” Iionyesha walirudi kwenye jambo lao la kwanza tena. Wakarudi pamoja na nguvu zao na wakarudi kwenye madhehebu ya Kipentekoste. Kifungu cha 15 cha—cha mlango uo huo. Vema.

¹⁶⁰ Kati ya nyakati hizo mbili walipata nguvu kidogo, katikati ya nyakati hizo mbili za fundisho la kimadhehebu la Kinikolai. Sasa, wakati Walutheri hapa walipokuwa wameunda, wakarudi katika Unikolai, wale maaskofu wakuu na kadhalika. Ndipo akaja Wesley, wakafanya askofu mkuu wa Canterbury na hawa wakuu wengine wote mbalimbali, kote kote juu ya hilo makanisani na kadhalika katika—katika wakati huo. Ndipo huku katika Upentekoste, wanarudi moja kwa moja kwenye kitu hicho hicho tena, madhehebu yao yote makuu, lile fundisho la Wanikolai. Lakini katikati ya nyakati hizi mbili Yeye aliufungua mlango na kulipa kanisa nguvu kidogo kufufuka vya kutosha hata likitikise kichwa chake, liangalie huko nje na kuona lilipokuwa, lipate ufunuo. Ligeuke, liona chochote (liliangushwa, mwajua), na muda si muda mwajua, lianze kutikisa kichwa chake na kuangalia kote na kutikisa kichwa chake.

¹⁶¹ Jambo lingine, nilikuwa nikiota juu ya hilo jana usiku. Charlie, nilifikiri nilikuwa nimempiga kuchakulo risasi; nikamwangusha kutoka kwenye tawi. Kisha nikamwona maskini bi kizee pale. Loo, alikuwa amenikasirikia sana, alikuwa aje, anipate. Naye kuchakulo huyu alikuwa na kamba ndogo nyeupe shingoni mwake. Basi maskini jamaa huyo alilala pale na kukitikisa kichwa chake mara mbili ama mara tatu, kisha akaniangalia, naye akatimua mbio kasi sana alivyoweza kwenda, moja kwa moja kurudi mwituni.

¹⁶² Mnajua, naye huyo bi kizee huenda alimaanisha kanisa. Sivyo? Akajaribu kunikanyaga, kwa njia fulani nikamwondokea. Na . . . Lakini, loo, nuru ndogo tu, bali ya kutosha kujua ku—ku . . . Najua nilishuka kwenda barabarani naye alitaka kunizuia huko chini, ndipo nikaigeuza Ford yangu upesi; walikuwa na trela nyuma yake, nikakishtua kitu hicho chote, nikatokea njia nyingine, asiye akanishika. Nikaepuka.

¹⁶³ “Sasa, unazo nguvu kidogo zilizosalia, kwa hiyo unataka kuzitumia nguvu hizi upate kugeuka nyuma kati ya hayo madhehebu mawili.” Mliona? “Walilitunza Neno Lake!” Angalia kifungu kinachofuata hapa sasa:

. . . wewe unazo nguvu kidogo, nawe umelitonza neno langu . . .

¹⁶⁴ “Umelitonza Neno Langu,” hivyo ndivyo walivyopata nguvu zao. Hivyo ndivyo walivyopata ufunuo wao. Wale walioishika Biblia wakati Luther alipoichapisha Biblia, ndipo ikaja kupitia

wakati wa Wesley na kadhalika, wakalishika pale na kulitunza Neno; nao wakauona ufunuo wa Yesu Kristo akiwa ni Mungu aliyefanyika mwili miongoni mwetu, na ubatizo wa maji katika Jina la Yesu, kwa hiyo wakaingia moja kwa moja ndani yake. Haya basi. Ndipo waka—wakalipata Jina Lake basi. Mnaona? Mbona, ni dhahiri tu kama . . . dhahiri kuliko kusoma gazeti. Mnaona? Ninii tu. . . Wala huwezi kulikana, maana ni hili papa hapa. Limeonyeshwa papa hapa katika Biblia, nalo hili papa hapa, nasi tuna. . . Ni historia. Hapo ndipo hasa kanisa la Kipentekoste lilipoanza na kupata jina lake, yapata mwaka wa 1908, '10, '12, mahali fulani hapo, likianza kuanguka.

165 Sasa, vema:

. . . *wala hujalikana jina . . . hujalikana jina langu.*

166 Sasa, ninapenda hilo. Yeye anazo fu—funguo za Daudi sasa, Yeye anaweza kulitunza Neno Lake na—na kukuweka katika Ufalme. Jina Lake lilikuwa limefunuliwa. Walitoka kwenye kanisa lililokuwa na “jina kwamba walikuwa wamekufa,” na sasa waliingia katika kanisa ambalo lina Jina, hiyo ni kusema, lina Uzima. Mnaona? Wametoka kwa, “Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu” lililokufa. Jina la “Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu,” hilo hata halina maana. Mnaona, limetolewa hapo kwa ajili ya ufunuo. Kitabu Chake chote kimeandikwa juu ya ufunuo. Hivyo ndivyo ilivyo, Yeye hujifunua Mwenyewe.

167 Sasa Yeye alisema, “Enendeni mkawabatize watu katika Jina la Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu,” Mathayo 28:19. Sasa, ni gani moja kati ya majina hayo utakalotumia? Sasa, karibu wautatu wote hubatiza, “Katika jina la Baba, katika jina la Mwana, katika jina la Roho Mtakatifu.” Hilo hata si la Kimaandiko. Mwulize mtu yeyote. Angalieni kama si. . . Ni katika *jina*, umoja, sio *majina*. *Jina!* Jina la Baba na Mwana na Roho Mtakatifu. Mnaona? Vema. Baba si jina; Mwana si jina; Roho Mtakatifu si jina. Kwa hiyo ni kitu gani? Kitu kilichokufa! Hakuna jina kwake. Lakini kupitia kwa sifa hizo zilizokufa. . .

168 Kwa Uzima wa Kristo, linafunua. Naye Petro hapana shaka alikuwa na. . . Alikuwa amesimama pale pale akiwa na zile funguo za—za Ufalme wa Mbinguni mkononi mwake, nao huo Ufalme ni Roho Mtakatifu; zikining’inia ubavuni mwake, zile funguo za Ufalme. Kwa maneno mengine, ufunuo, maana Yesu alimwambia. Loo, ndugu, hivi hamwoni hilo? Petro alikuwa ndiye aliyebatizwa na ufunuo wa Kweli. Naye huyo hapo amesimama papo hapo, naye akamsikia Yesu akisema, “Enendeni basi, mkawafundishe mataifa yote, mkiwabatiza katika Jina la Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu.”

169 Petro akageuka na kusema, “Bwana, hakika ninazo funguo hapa. Nimepata ufunuo wa kile hilo lilichomaanisha, maana ninajua Baba si jina, Mwana si jina, na Roho Mtakatifu si jina, ila

ninajua Jina hilo ni gani.” “Kwa hiyo ninakubatiza katika Jina la Bwana Yesu Kristo.” Amina. Whiu! Hiyo ni kweli.

¹⁷⁰ Sasa, ni kama tu ulikuwa ukisoma hadithi ya mapenzi. Nawe. . . Hicho ndicho kitabu cha mwisho cha Mathayo, sehemu ya mwisho ya Mathayo. Kama ulichukua kitabu cha mapenzi, baadhi yenu kina mama. . . Ninajua hamfanyi hivyo, hakika msingefanya hivyo; la, la. Mnaona? Lakini kama ulifanya hivyo wakati ulipokuwa mwenye dhambi, unaona, ukaichukua hadithi hiyo huko chini kwenye. . . unajua, ulipokuwa ni maskini msichana mdogo, nawe ukaichukua hadithi hii, nayo ikasema, “Yohana na Mariamu waliishi kwa furaha tangu hapo na kuendelea.” Huh! Kwani Yohana na Mariamu ni akina nani? Sasa, kuna njia moja tu kwako kujua Yohana na Mariamu ni akina nani, hiyo ni, rudi mwanzoni mwa kitabu ukasome. Hiyo ni kweli?

¹⁷¹ Vema, basi katika kitabu cha mwisho cha Mathayo, kifungu cha mwisho, ambapo Yesu alisema, “Enendeni basi, mkawafundishe mataifa yote, mkiwabatiza katika Jina la Baba, na la Mwana, na Roho Mtakatifu, mkiwafundisha kuyashika yoyote niliyowaamuru.” Sasa, kama—kama Baba si jina, na Mwana si jina, na Roho Mtakatifu si jina, afadhali mrudi mwanzoni mwa hicho Kitabu. Mnaona? Sasa, kama tukirudi mwanzoni mwa Kitabu, mlango wa kwanza wa Mathayo, mnapata hili.

¹⁷² Ningetaka tu kutoa maelezo haya madogo hapa kwa kuwa huenda kukawa na mtu fulani hapa ambaye kamwe hajawahi kuliona. Angalieni hili. *Huyu* ni Baba, *huyu* ni Mwana, na *huyu* ni Roho Mtakatifu. Sasa, angalieni kwa makini. Baba, Mwana, Roho Mtakatifu. Hivyo ndivyo Yesu alivyosema katika Mathayo 28:19. Hiyo ni kweli? Baba, Mwana, Roho Mtakatifu. Sasa, *huyu* ni nani? Baba? Sikilizeni enyi darasa. Baba, Roho Mtakatifu, Mwana. Sasa, *huyu* ni nani? Roho Mtakatifu. *Huyu* ni nani? [Kusanyiko linasema, “Baba.”—Mh.] *Huyu* ni nani? [Kusanyiko linasema, “Mwana.”] Mwana. Vema. Sasa, *huyu* alikuwa ni Baba wa Nani? Yesu Kristo. Hiyo ni kweli?

¹⁷³ Sasa, Mathayo, mlango wa kwanza, kifungu cha 28, hebu na tulisome. Tutaichukua hiyo hadithi ya mapenzi sasa tuone jinsi inavyosomeka. Tutaona Jamaa *huyu* alikuwa ni Nani—Nani ambaye, wa, ambaye alisema, “Enendeni mkawabatize katika Jina la Baba, na la Mwana, na Roho Mtakatifu.” Vema. Sasa, mlango wa kwanza wa Mathayo unaanza na ukoo:

Kitabu cha vizazi vya Yesu Kristo, mwana wa Daudi, mwana wa Ibrahimu.

Ibrahimu alimzaa Isaka; . . . Isaka akamzaa Yakobo; . . .

174 Na kuendelea, kuendelea, na kuendelea, moja kwa moja hata kufikia kwenye ki—kifungu cha 18. Sasa, mnaona, endeleeni hapa chini kwenye kifungu cha 17 na . . .

Basi vizazi vyote tangu Ibrahimu hata Daudi vilikuwa vizazi kumi na vinne; na tangu Daudi hata ule uhamisho wa Babeli . . . vizazi kumi na vinne; na . . . uhamisho wa Babeli hata Kristo vilikuwa vizazi kumi na vinne.

Kuzaliwa kwake Yesu Kristo kulikuwa hivi: Wakati . . . Mariamu mama yake alipokuwa ameposwa na Yusufu, . . .

175 Mnasoma nyuma yangu? Sikilizeni kwa makini:

. . . Wakati . . . Mariamu mama yake alipokuwa ameposwa na Yusufu, . . . alionekana ana . . . kabla hawajakaribiana, alionekana ana mimba kwa uweza wa Mungu Baba.

176 Hilo linasomeka hivyo? Alionekana ana mtoto wa nani? [Kusanyiko linasema, “*Roho Mtakatifu!*”—Mh.] Vema, nilifikiri mtu fulani alisema *huyu* alikuwa ndiye Baba Yake. Sasa, kama Roho Mtakatifu ni mtu mmoja, naye Baba ni mtu mwingine, basi Yeye alikuwa na baba wawili. Mna kitu gani? Mtoto haramu. “Loo,” mlisema, “yeye . . . hao waliteleza tu kidogo na kuchapisha vibaya hapa.” Vema:

Naye Yusufu mumewe, kwa vile alivyokuwa mtu wa haki, . . . asitake . . . asitake kumwaibisha, aliazimu kumwacha kwa siri.

*Basi alipokuwa akifikiri hayo, tazama, malaika wa Bwana alimtokea katika ndoto, akisema, Yusufu, mwana wa Daudi, usihofu kumchukua Mariamu mkeo: maana mimba yake ni kwa uweza wa . . . [Kusanyiko linasema, “*Roho Mtakatifu!*”]*

177 “Kinywa cha mashahidi wawili au watatu, kila neno na lithibitishwe.” Mnaona? Uh-huh. Roho Mtakatifu alikuwa ndiye Baba Yake. Vema, Yeye alisema “Mungu” alikuwa ndiye Baba Yake. Sasa, kama hao ni watu wawili mbalimbali, ni yupi aliyekuwa baba Yake? Angalia mahali unapojiweka. Unajining’iniza tu huko nje katikati ya katikati ya hewa. Unaoona? Sasa, huna budi kusema kwamba Roho Mtakatifu ni Mungu Mwenyewe! Ni Roho Mtakatifu, ambaye ni Mungu. (Sasa, unao wawili sasa, badala ya watatu.) Vema.

178 Vema, kifungu cha 21:

. . . mimba yake . . . (Ni nani aliyeweka . . . Ni nani Yule aliyempa mimba hii? Roho Mtakatifu. Vema.)

Naye atamzaa mwana, nawe utamwita jina (Jina) lake YESU: maana yeye ndiye atakayewaokoa watu wake na dhambi zao.

...hayo yote yamekuwa,...Sasa hayo yote yamekuwa, ili litimie neno lililonenwa na Bwana kwa ujumbe wa nabii, akisema,

Tazama, bikira atachukua mimba, naye atazaa mwana, nao watamwita jina lake Imanueli...yaani,... Mungu pamoja nasi.

179 Jina Lake lilikuwa ni nani? Sasa, Yohana na Mariamu ni akina nani walioishi kwa raha mstarehe tangu hapo na kuendelea? Jina la Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu ni lipi? Yesu alipozaliwa duniani, Yeye alikuwa ni Kristo Bwana. Katika kutahiriwa Kwake (siku nane baadaye) mama Yake alimpa Jina na baba Yake akampa Jina la “Yesu.” Alikuwa ni Yesu Kristo, Bwana Yesu Kristo, wakati huo.

180 Yeye alikuwa ni Bwana! Wakati alipozaliwa, Yeye alikuwa ni Kristo Bwana. Halafu alipopokea Jina Lake la “Yesu,” hilo lilimfanya Yesu Kristo aliye Bwana. Hilo ndilo lile hasa lililofunuliwa kwa Petro, yeye alijua Yohana na Mariamu walikuwa ni nani hapo aliposema, “Nendeni mkabatize katika Jina la Baba, Mwana, Roho Mtakatifu.” Kwa hiyo, ingeweza kufunuliwa kwa sababu Yesu alijua ya kwamba Petro alikuwa na karama ya ufunuo, Yeye alijua, kwa sababu ilikuwa tayari imefunuliwa kwake na Roho aliye juu. Basi wakati Mungu anapooa ya kwamba mtu anaweza kuupokea ufunuo utokao juu, Yeye anaweza kumtumaini mtu huyo, kufanya jambo fulani naye; wakati limefunuliwa kwake, kwa sababu Yeye alisema, “Hakuna mtu anayeweza kulifunua hili ila Baba Yake.” Mungu Ndiye tu awezaye kulifunua, Naye alijua Petro katika... alikuwa akiwasiliana na Roho. Kwa hiyo yeye . . .

181 Petro alijua ule ufunuo, ndipo akapanda kule na kusema, “Tubuni, mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi zenu.”

182 Sasa, siku chache tu kabla ya hapo, Yesu alimwambia Petro, (Wakati ule ule alipomwambia huo ufunuo ulikuwa ni Nani, “Juu ya Mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu, wala malango ya kuzimu hayatalishinda.”), “Nami nakwambia kuwa wewe ndiwe Petro, nami nitakupa funguo.” Loo! “Funguo za Ufalme! Nitakupa funguo. Lolote utakalolifunga duniani, nitalifunga Mbinguni. Utakalolifungua duniani, nitalifungua Mbinguni.”

183 Ndipo kwenye Siku ya Pentekoste, kwenye kule kuzinduliwa kwa Kanisa, siku kumi baada ya Yesu kusema “enendeni mkabatize katika—katika Jina la Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu,” Petro kwa ufunuo wa kiroho alijua hapakuwapo na kitu kama jina la “Baba, Mwana, Roho Mtakatifu.” Vema, hakuna mtu mwingine aliyeliwazia hilo mpaka ule wakati wa Katoliki. Na kila mtu aliyebatizwa katika jina la “Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu” kwa kweli amebatizwa katika imani ya

Kikatoliki, (hiyo ni kweli) si katika ubatizo wa Kikristo. Kulikuwa . . . waliosalia.

184 Sasa, kwenye Siku ya Pentekoste, wote walijazwa na Roho Mtakatifu, na kunena kwa lugha na—na kutenda kama walevi. Nao walikuwa ni walevi, walilewa kwa Divai mpya. Ile Divai mpya iliyotoka Mbinguni, kutoka Kanaani iliyo juu. Ndipo wakati hao wote walipokuwa wakipiga shangwe na kupaza sauti na kutenda kana kwamba walikuwa walevi na kadhalika, Petro alisimama miongoni mwao na kuwaambia kwamba “Hawakulewa, bali walikuwa—walikuwa . . . Hili lilikuwa ni ile ambalo nabii alikuwa amesema lingetukia, ‘Yeye angeimwaga Roho Yake.’”

185 Na sasa wao—wao walisema, “Wanaume na ndugu zetu, tufanye nini? Wanaume na ndugu zetu, tufanye nini?” Hilo ndilo swali. “Tutampataje? Ni nani aliye na funguo?”

186 “Njoo hapa, Simoni. Unazo funguo, ziteo ubavuni mwako. Basi utasema nini? Sasa kumbuka, Yezu Kristo alisema, ‘Ukilifunga duniani, nitalifunga Mbinguni. Kama ukilifungua duniani, nitalifungua Mbinguni.’ Na kama Yeye ni Mungu, Yeye hana budi kulitimiza Neno Lake.”

187 Sasa, ninyi makasisi wa Katoliki, hebu mnionyeshe “msamaha wenu wa dhambi.” Kasisi wa Katoliki aliniambia wakati mmoja, kasema, “Hivi Yesu hakusema, ‘Yeyote mtakayemwondolea dhambi zake, zimeondolewa?’”

Nikasema, “Yeye alisema hivyo.”

“‘Yeyote mtakayemhesabia dhambi, zimehesabiwa?’”

“Naam.”

“Hiyo ni yeyote mtakayemsamehe, wamesamehewa; wowote msiowasamehe, hawajasamehewa.”

Nikasema, “Hivyo ndivyo lilivyosema kweli.”

Akasema, “Basi hivi si Kristo alilipa Kanisa Lake, ambalo sisi ni Kanisa Lake, mamlaka ya kusamehe dhambi duniani?”

188 “Hakika alilipa.” Nikasema, “Sasa, kama mtawasamehe vile walivyowasamehe, nitaambatana nanyi.” Naam. Nikasema, “Waliwasamehe kwa njia gani? Je, waliwaambia, ‘Nendeni mkafanye vitubio ya siku tisa ama chochote kile, ama jinsi mfanyavyo?’”

189 La, bwana. Petro alisema, “Tubuni!” Amina. Huo hapo ule ufunguo, “Tubuni, kila mmoja wenu, mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi zenu, na ndipo mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.” Huo ufunguo ukafanya “klik” duniani, na ukafanya “klik” Mbinguni. Jambo ndilo hilo.

190 Hiyo ndiyo sababu wakati Paulo alipokutana na wengine ambao walikuwa tayari wamebatizwa na mtu yule yule

aliyembatiza Yesu, yeye alisema, “Je, mmempokea Roho Mtakatifu tangu mlipoamini?”

Wakasema, “Hata hatujui kama kuna Roho Mtakatifu.”

Akasema, “Kwa *nini*...” Hebu chukua neno lako la Kiyunani, alisema, “Mlibatizwa *vipi*?”

Wakasema, “Wa Yohana.”

Kasema, “Huo hautafanya kazi tena. Mbinguni tayari imefungwa. Hamna budi kuja; mkabatizwe katika Jina la ‘Yesu Kristo.’”

¹⁹¹ Kwa hiyo waliposikia haya, wakabatizwa tena katika Jina la Yesu Kristo. Basi walipobatizwa, Paulo aliweka mikono yake juu yao, Roho Mtakatifu akaja juu yao, wakanena kwa lugha na kutabiri.

¹⁹² Loo, ndugu, hiyo ni kurudi huko mwanzo. Hiyo ni hakika. Huo ndio “mlango uliofunguliwa” uliowekwa papa hapa. Kijeografia ni kweli, Nuru za jioni, na kila Andiko katika Biblia linaelekeza kwake hasa.

¹⁹³ Tungeweza kusimama hapa kwa saa kadhaa, nami nina dakika kumi na tano zaidi, na yapata matamshi thelathini na matano mbalimbali ya kutoa hapa. Basi endapo hatutaweza, tutayapata asubuhi tusipoyapata usiku wa leo. Vema.

¹⁹⁴ Sasa, vema:

...wala hapana aufungaye; kwa kuwa unazo nguvu kidogo, nawe umelitunza neno langu... (Vema)... wala hujalikana jina langu.

¹⁹⁵ Hapo tumelipata! “Hukulikana Jina Langu.” Jina lilikuwa limefunuliwa, wakaondoka kwenye dhehebu la kale la Sardi, nao walikuwa wameingia kwenye Kanisa lililo hai.

¹⁹⁶ Sasa hebu tuchukue kifungu cha 9. Sasa, tutaangalia sasa, tunafikia kwenye kitu ambacho ni cha hatari sana:

Tazama, nitawafanya walio wa sinagogi la Shetani, wasemao kwamba ni Wayahudi, nao sio, bali wasema uongo. Tazama, nitawafanya waje kusujudu mbele ya miguu yako, na kujua ya kuwa nimekupenda.

¹⁹⁷ Kunayo shibe ya usiku mzima, papo hapo. Angalieni! Hao ni nini sasa? Hao aliozungumza nao, waliokuwa wamelipata Jina Lake baada ya wakati huu wote *hapa* chini, wakaingia katika Yesu Kristo “Mlango uliofunguliwa” (wanalo Neno la Uzima, wamejazwa kwa Roho Mtakatifu), na sasa Yeye alisema, “Kunao wale miongoni mwenu walio katika sinagogi la Shetani.”

¹⁹⁸ Sasa, ndugu yangu, kama ungetaka tu kurudi kwe—kwenye Pargamo, kwenye Ufunuo 2:13, kwa dakika moja tu, na hebu niwaonyeshe tu hapa kile hilo lilicho: dhehebu.

Nayajua matendo yako, na ukaapo, ndipo penye kiti cha enzi cha Shetani:...

199 Haya basi. Laodikia hiyo . . . ama, ninamaanisha wakati huo wa kanisa la Nikolai ambako walikuwa wameunda dhehebu. Basi tazama, kuonyesha ya kwamba walikuwa ni kanisa, sinagogi, kanisa, kanisa la kimadhehebu. Loo, ndugu! “Sinagogi la Shetani.” Basi, kazi za dhehebu ni za ibilisi! Sio Wakristo, sasa, kumbukeni, wao ni Wakristo, bali dhehebu lenyewe. Vema.

200 Sasa, hivi mliona Yeye alisema, “Mnao wale miongoni mwenu wanaosema wao ni ‘Wayahudi,’ bali mmewapata kuwa ni waongo.”

201 Sasa, kumbukeni, yule malaika mkuu . . . Sasa yeye anasema na nani? Kanisa hili la mwisho, mlango huu uliofunguliwa kati ya makanisa hayo mawili.

202 Sasa, wakati wa kwanza wa kanisa ulifundishwa na nani? Paulo. Sasa hebu twende kwenye Warumi 2:29 tuone Myahudi ni nani, kusudi mpate kujua hakika siyo—siyo mawazo yangu mwenyewe juu yake. Warumi mlango wa pili, na kifungu cha 29, cha Warumi. Vema, haya basi:

Bali yeye ni Myahudi aliye Myahudi kwa ndani; na tohara ni . . . ya moyo, na katika roho, si katika andiko; ambaye sifa yake ha—haitoki kwa . . . ambaye sifa yake haitoki kwa wanadamu, bali kwa Mungu.

203 Myahudi ni—ni nani? Roho, Mkristo aliyejazwa na Roho Mtakatifu! “Ninajua ya kwamba mko hapa chini baada ya wakati huo wa utakaso wanaosema ‘walimpokea Roho Mtakatifu,’ bali yeye alilisema, sikulisema mimi.” Walisema walikuwa na Roho Mtakatifu pasipo ishara zinazofuata, bali Yeye alisema, “Ni waongo.” “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Huwezi kumfanya Yeye aseme uongo. Loo, ndugu! Hilo linakupofusha huku, huku. Unaona? Loo, jamani!

Nitaninii . . . Tazama, nitawafanya walio wa sinagogi la Shetani, wasemao kwamba ni Wayahudi, (“Wasemao ni ‘Wakristo waliojazwa na Roho,’ wasemao; sinagogi, dhehebu. Nitawafanya wasemao wana ‘Roho Mtakatifu’; na wote wameunda dhehebu—wamejiundia dhehebu huko juu. Hata hawana ufunuo bado!” Mnaona? Vema.) . . . Nitasema . . . hao wasemao kwamba ni Wayahudi (ni Wakristo), nao sio, bali wasemao uongo; Tazama, nitawafanya . . . waje kusujudu mbele ya miguu yako, na kujua ya kuwa nimekupenda.

204 Papa hapa itabidi linifunukie tu katika ujumbe wa asubuhi hii. Hao ni wale wanawali waliolala papo hapo. Mnaweza kuliona? Ilikuwa ni wakati gani? Kwenye wakati wa mwisho. Loo, walipotoka nje. Hawa hapa . . . Mnaona? Wamehesabiwa haki kwa imani, wakatakaswa. Wakahesabiwa haki kupitia kwa ujumbe wa Luther, wakatakaswa kupitia hapa, bali wakaukosa “Mlango uliofunguliwa.” Mnaliona? Wakahesabiwa haki kwa imani, kupitia Luther; wakatakaswa, kupitia wakati wa Wesley.

205 Wengi wao ni Wanazarayo wa thamani, Wapilgrim Holiness, Methodisti ya Kiwesley, na kadhalika, wote wanaishi maisha mazuri, safi, yaliyotakaswa, nao wanadhani wanaye Roho Mtakatifu; na kumsikia jamaa akizungumza kwa lugha, ama kitu fulani, watamcheka, watamdhahaki, na kusema, “Ni ya ibilisi.” Ndugu, ulitia muhuri maangamizi yako wakati ulipofanya hivyo. Ulimkufuru Roho Mtakatifu, ambalo halisameheki.

206 Vema, mnasema, “Sisi ni wafuasi wa kanisa la Kwanza.” Sijali wewe ni mfuasi wa makanisa mangapi. Halina uhusiano wowote na Neno la Mungu, na “usiondoe wala kuongeza.” Hiyo ni kweli, “Masinagogi ya Shetani!”

207 Natumaini siwaudhi. Ni—ninachukia tu kuzungumza namna hiyo, bali kuna—kuna kitu Fulani ndani yangu kinachonihamasisha kulifanya. Sijui ni kwa nini mimi hulifanya. Mnajua sipendi kufanya hivyo. Ninajisikia tu vibaya sana ninapolisema, bali hata hivyo sina budi kulisema. Kuna kitu Fulani mle ndani kinachonifanya kulisema. Daima nilichukia kuwakemea wanawake, na—najisikia ninii sana. . . Mwanamke anaweza kulia, nami ninajisikia tu vibaya. Ni—ninachukia tu kuwakemea wanawake, bali kuna kitu Fulani mle ndani kinachonifanya nilifanye. Mnaona? Mwanamke mtovu wa uadilifu (Loo, jamani!), kamwe siwezi kulivumilia. Kwa sababu, kuna kitu Fulani ndani kinachonifanya nilifanye, Roho Mtakatifu.

208 Nami ninaangalia hapa chini kwenye Neno, ninawazia, “Bwana, kama nimekosea, nionyeshe. Usiniache nifanye hilo kusudi tu niende namna hiyo. Watu hawataninii. . . Sitaninii. . . Ninawapenda watu, Wewe unajua nawapenda. Usiniache nimuudhi mtu yeyote, Mungu, Wewe unajua nisingefanya hivyo.”

209 Lakini Roho Mtakatifu anasimama na kusema, “Simama kwenye Neno hilo! Dumu hapo! Kaa papo hapo kwenye Neno hilo!”

210 Nami nasema, “Naam, Bwana. Kama ni. . . Wewe Ndiwe rafiki yangu mwema kuliko wote. Wewe ndiwe pekee ambaye mimi. . . Wewe ndiwe rafiki yangu halisi ambaye ataninii. . . Yule pekee atakayenisaidia wakati maisha haya yatakapokuwa yakififia, kwa hiyo nitasimama moja kwa moja pamoja na Nawe, Bwana.”

211 Mimi hapa naja. Simaanishi kuudhi, naomba msinichukue vibaya wakati ninapoyakemea hayo madhehebu na kadhalika. Zamani sana kabla sijajua lolote kuhusu hili, maishani mwangu mwote, nimeyakemea. Kamwe sikuyaamini, hiyo ndiyo sababu nisingejiunga nayo. Na. . . Vema. Mungu ashukuriwe kwa kuniweka mbali nayo!

Tazama, nitawafanya walio wa sinagogi la Shetani, wasemao kwamba wamejazwa na Roho, nao sio, bali. . . uongo; nami nitawafanya waje. . . kusujudu mbele ya miguu yako. . .

212 Hivi hamkumbuki yule mwanamwali aliyelala wakati alipoamka? Sasa, kumbukeni, yeye alitwaje? Kunao kumi waliotoka kwenda kumlaki Bwana-arusi. Hiyo ni kweli? Watano walikuwa wenye busara, walikuwa na Mafuta kwenye taa yao. Ni wangapi wanaojua mafuta yanawakilisha nini katika Biblia? Roho. Sasa, mmoja asingeweza kusema, “Wewe hujatakaswa, wala mimi. . .” Wote walikuwa wametakaswa, kila mmoja yao. Wote walitakaswa; bali watano walikuwa wenye hekima vya kutosha (kuwa na hekima ya ufunuo) kuushika huo Mlango, mnaona, kujazwa na Roho. Walikuwa na Mafuta kwenye taa zao, na hao wengine hawakuwa na Mafuta. Basi walipoamshwa, mbona, hawa hapa wanawajia, kasema, “Loo! Loo! Nipeni Roho Mtakatifu wenu kidogo, Mafuta. Nipeni kidogo!”

213 Kasema, “Naam, samahani, dada, ninayo tu ya kunitosha mimi. Hakika sina yoyote ya ziada.”

214 Kwa hiyo. . .basi wakati. . .Yeye alisema, “Nendeni mkaombe vya kutosha.” Ndipo walipokuwa wameondoka kwenda kununua kidogo, Bwana-arusi akaja na wakaingia kwenye ile Karamu ya Arusi; nao wakaacha nje, ambako watapitia kwenye ule wakati wa Dhiki ya. . .Tazameni tu katika vifungu vichache vifuatavyo, mtaona waliingia moja kwa moja kwenye ule wakati wa Dhiki. Mnaona?

215 Sasa, wale waliolala. . .Tatalichukua hilo asubuhi. Naam, ninaamini ingekuwa bora zaidi kidogo kama tungengojea hilo, maana tunafikia hapa chini sasa tukikaribia tu wakati, vema, wa kufunga.

216 Sasa hebu tuone:

Tazama, nita. . .

Walikuta kwamba hao ni waongo, kwamba hawana Roho Mtakatifu.

217 Jambo moja tu dogo hapa, tafadhalini, wakati tukiwa sote pamoja. Yuda Iskariote, kama nilivyosema jana usiku, alikuwa ni mwana wa upotevu. Biblia ilisema, “Yeye alizaliwa mwana wa upotevu.” Ndipo wakati yeye. . .Naye Yesu Kristo alizaliwa Mwana wa Mungu. Ndipo, Mungu aliishi katika Kristo. Hiyo ni kweli? Nani. . .Shetani aliishi ndani ya Yuda. Ikiwa Yeye alikuwa ni Mwana wa Mungu, aliyezaliwa Mwana wa Mungu, Mwana wa Mungu aliyefanyika mwili; basi Shetani alizaliwa mwana wa upotevu, alikuwa aliyefanyika mwili. . .mwana wa upotevu, Shetani, ibilisi.

218 Sasa, kama ukitazama, alijiunganisha na Yesu, akawa mmoja wao. Mnaona? Sasa, sababu ya yeye kufanya hivyo,

ni kusudi apate udanganyifu huo ambapo angeweza kuingia kanisani siku hizi. Sasa, Yesu alisema, “Hayo masinagogi ni ya Shetani.” Loo, jamani! Hilo liliingia? Hayo ni masinagogi ya Shetani! Huyo ni Yuda akijifanya kuwa Mkristo.

219 Jambo kuu la Yuda lilikuwa ni nini? Lilikuwa ni pesa. Mvuto mkubwa sana wa vitu hivi siku hizi ni pesa. Hebu angalieni Assemblies of God, wakijenga jengo la dola milioni sita huku, huku wakifundisha “Bwana yuaja mara moja.” “Loo, mabomu yako kwenye mabanda kutulipulia mbali,” na huku wanajenga jengo la dola milioni sita. Loo, jamani. Vema, matajiri wala hamna haja. . . Tatalipata hilo kesho usiku, sasa, Bwana akipenda.

220 Sasa angalieni hapa. Loo, angalieni jinsi makanisa yalivyo makubwa, haya mashirika makubwa. Wanakusanya pesa zao pamoja na. . . Loo, rehema! Wanakuwa tu wa mabilioni. . . hata wanazo fedha, mashirika ya mikopo miongoni mwao, na kila kitu. Wakikopesha pesa na kadhalika, hayo makanisa. Ndugu, hilo halisikiki kama la kimitume kwangu mimi.

221 Petro alisema, “Sina fedha wala dhahabu, bali kile nilicho nacho. . .” Nipe Hicho, na uzichukue fedha zako zote. Hiyo ni kweli. “Fedha na dhahabu sina, bali nilicho nacho nakupa: Katika Jina la Yesu Kristo. . .” Hicho ndicho alichokuwa nacho, ufunuo Wake. “Nakupa: Katika Jina la Yesu Kristo simama utembe.”

222 Vema, sasa tunaona hapa ya kwamba walikuwa ni wa “sinagogi la Shetani.” Sasa, wangewezaje kuwa? Sasa, Yuda wakati alipokuja. . . Sasa angalieni! Yapata tu wakati Yesu alipokuja jukwaani, Yuda alikuja jukwaani. Mnaliona hilo? Na yapata wakati tu Yesu alipoondoka jukwaani, Yuda aliondoka jukwaani. Yapata wakati Roho Mtakatifu aliporudi jukwaani tena, Yuda alirudi jukwaani. Roho ya mpinga-Kristo, kufanya kazi, pia wana wa kuasi, wasioijali Biblia, bali wakijali dhe—dhehebu. Mnaona? Nao wakajifanyia sinagogi! Ndipo Yesu akasema hapa, “Ni sinagogi la Shetani.” Wapi? Wakiketi huku chini kabisa katika wakati huu *hapa*. Lilianzaje *hapa* nyuma? Kwa dhehebu. Hilo ndilo jambo lile lile lililofanya *hapa* chini. “Sinagogi la Shetani.” Mnalipata?

223 “Sinagogi la Shetani,” Yeye alisema, “ambao wanasema wamejazwa na Roho.” Sasa, wangewezaje kusema hivyo?

224 Yuda, wakati alipokuwa hapa duniani, yeye alikutana na Yesu, akakiri ya kwamba alikuwa ni mwaminio wa Yesu, kisha akawa mweka hazina, akibeba pesa zote. Hiyo ni kweli? Nyote mnajua hilo. Sasa, kama alimwamini Yesu Kristo, alikubali (kwa uongo) kuhesabiwa haki. Hiyo ni kweli? Katika Warumi 5:1, “Basi tukiisha kuhesabiwa haki kwa imani.” Hiyo ni kweli. Vema.

225 Sasa, halafu jambo lingine, katika Yohana Mtakatifu 17:17, Yesu aliwatakasa kwa ile Kweli, Yeye alisema, “Neno Lako ndilo Kweli,” Naye alikuwa ni Neno.

226 Kisha akawapa nguvu dhidi ya pepo wachafu; kutoka kwenda kufanya ibada za uponyaji, na kuwatoa pepo, na—na kufanya kila namna ya miujiza. Ndipo waliporudi, Yuda akiwa pamoja nao. . . Sasa angalieni, Nazarayo, Methodisti ya Kiwesley! Wakarudi, wakishangilia, na wenye furaha kuu, na kumsifu Mungu, na kupaza sauti kwa sababu pepo walikuwa wanawatii. Naye Yesu akasema, “Msifurahie kwa sababu ibilisi wanawatii, bali furahini kwa kuwa majina yenu yameandikwa katika Kitabu cha Uzima.”

227 Basi kumbukeni Yuda alikuwa mmoja wao! Mnaona, yeye angeweza kulidanganya kanisa kufikia umbali huo. Ametenda kazi moja kwa moja kupitia kwenye mistari hiyo, mwajua, bali ilipofikia kwenye Pentekoste yeye alionyesha rangi zake. Hivyo ndivyo vile hasa alivyofanya katika lile la Asilia, katika kanisa la Methodisti, na yale aliyofanya katika kanisa la Kilutheri, na yale aliyofanya katika kanisa la Nazarayo, na Churches of God na hayo mengine, akaja moja kwa moja hadi kwenye utakaso; ilipofikia kwenye ubatizo wa Roho Mtakatifu kuna kwa lugha, na kuwa na ishara na maajabu, walilihukumu.

228 Watapitia kwenye njia ya uponyaji wa Kiungu kwa ajili yenu. Hakika, Yuda alifanya hivyo pia. Mnaona? Lakini wakati. . . Kuna uponyaji mwingi wa Kiungu. Wako njiani leo hii, ndugu, wakisimama kwa saa mbili na kusema, “Mazao yenu yatakauka kama huwapi dola hamsini kila usiku, kila mmoja wenu.” Na upuuzi huo wote wa namna hiyo, huyo ni ibilisi. Hakika ndiye. Ninaamini katika uponyaji wa Kiungu kwa moyo wangu wote. Lakini upuuzi huo ni wa ibilisi, kabisa, huo ni wa ibilisi. Sijali yale unayoweza kufanya, au ni zaidi sana vipi; Yuda aliwatoa pepo, pia.

229 Yesu alisema, “Wengi watakuja Kwangu katika siku hiyo, waseme, ‘Bwana, Bwana, mimi. . . hivi sikutoa pepo katika Jina Lako na kufanya kazi kuu?’”

230 Yeye akasema, “Kama mlizifanya, sina habari. Ondokeni kwangu, eni mtendao maovu, sikuwajua.” Hakika.

231 Loo, ndugu, “mlango ni mwembamba, na njia imesonga, bali ni wachache watakaopata.” Tunazungumza kuhusu “wachache” hawa kwa sababu tuko kwenye wakati wa mwisho ambapo hapana budi watakuwa ni wachache tu. Lipokeeni, tafadhalini, ndugu zangu!

232 Msifikiri kwamba ninasimama hapa. . . Afadhali ningeninii. . . Kama ingekuwa ni mimi, ninge—ningeninii. . . Kwangu mimi, ningeweza kupatana kwa nafsi yangu na kusema, “Hebu tuchukue Assemblies of God ama shirika fulani, tujiunge tu nalo na kuendelea pamoja nao.” Lakini, Loo, ndugu, ole

wangu kama nikifanya hivyo! Ole wangu! Ninajua vema kuliko hivyo. Mungu angenipeleka kuzimuni kwa kufanya kitu kama hicho. Naam, bwana. Kama nina ninii. . . Ikinibidi kutia muhuri ushuhuda wangu kwa maisha yangu, itanibidi tu kuutia, hivyo tu. Kwa sababu kuna kitu Fulani ndani yangu, nisingeweza kufanya hivyo hata iweje.

²³³ Ninajua hii ni Kweli, nami sina budi kuyatetea yaliyo Kweli, nayo Biblia inayaunga mkono. Dhehebu linayapinga, bali Biblia inasema kwamba ni kweli. “Neno la kila mtu na liwe uongo, na Lake kweli.” Hilo ni Kweli, hilo Ndilo, dumuni tu na Hilo.

. . . wafanya . . . sinagogi la Shetani . . . (Vema) . . . Nao watajua . . . waje mbele ya miguu yako, na . . . kujua ya kwamba . . . nakupenda wewe.

Kwa kuwa umeyashika maneno ya subira yangu, Mimi nami nitakulinda utoke katika saa ya kujaribiwa . . .

²³⁴ Angalia sasa, kuonyesha ya kwamba huu si wakati wa Kimethodisti ninaozungumzia, hata hivyo, ni mpandano. Angalieni! Mko tayari kusikiliza? Kila mtu? Sikilizeni kwa makini sasa:

Kwa kuwa umelishika neno langu la subira yangu, Mimi Nami nitakulinda (maskini hao wachache waliosalia) utoke katika saa ya kujaribiwa, wakati . . .

²³⁵ Kanisa litafikia mahali ambapo itakubidi kuingia kwenye dhehebu hili ama—ama uwe. . . itakubidi ku—utakuwa nao, ndugu. Hivyo tu. Ama utajiundia dhehebu au utachukua alama ya mnyama, ama kuchukua. . . Ama utajiundia dhehebu, au ujiunge na dhehebu (ambapo kweli alama ya mnyama inakuja), maana ni kususia. Mnaona?

. . . kuujilia . . . iliyo tayari kuujilia ulimwengu wote, kuwajaribu wakaao juu ya nchi.

Tazama, naja upesi: shikilia sana kile ulicho nacho, asije mtu akaitwaa taji yako.

²³⁶ Sasa hili “jaribio” kuu, saa ya kujaribiwa itakayokuja kuwajaribu walimwengu wote, inaingia katika ile Dhiki. Katika dakika chache tu tutaiona. Inaingia katika ile Dhiki, nayo ile Dhiki haikuja katika siku za Wesley. Kwa hiyo tuko katika wakati gani? Huu “Mlango” umewekwa mbele ya nini? Uko katikati ya Wesley na ninii. . . mahali kanisa linakoelekea sasa hivi, na liko ndani tayari, kwenye wakati wa Laodikia. Lakini mahali hapa padogo papa hapa ndani, katika miaka thelathini na mitano, arobaini iliyopita, imekuwa ni “mlango uliofunguliwa” umewekwa moja kwa moja mbele za watu wapate kuingia, naye Mungu atawachukua Waliosalia na kuwatia muhuri. Nao wataingia kwenye uvuguvugu ndipo Yeye atawatema watoke kinywani Mwake. Kazi itafupishwa, Kanisa linyakuliwe, naye huyu hapa mpinga Kristo akiingia kwa ajili

ya maangamizi. Kikamilifu kabisa, linalingana na Biblia nzima moja kwa moja kote. Vema, sasa.

²³⁷ Basi hapa ndipo kuonekana kwa mwanawali aliyelala pia. Hapa inathibitisha ya kwamba ule wa mwisho wa nyakati za kanisa unajongea kwenye sehemu ya kwanza ya Pentekoste, kwa kuwa wanaingia kwenye ile Dhiki Kuu ambayo itakuja katika . . . ambayo haikuja katika wakati wa Wesley.

²³⁸ Kifungu cha 11, vema, “taji ya Uzima.” Ki—Kifungu cha 11 kilisema:

Tazama, naja upesi: . . . (Ati nini? Upesi baada ya hili sasa, mnaona.)

Tazama, mimi. . . shika sana kile ulicho nacho (kishikilie kwa dhati), asije mtu akaitwaa taji yako.

²³⁹ “Taji” ni nini? Taji ni nini? Ni—ni—ni. . . *Taji* inamaanisha ya kwamba “una—una milki.” Wewe ni mfalme iwapo umevikwa taji. Unaona? Nasi ni wana wa Mungu wakati tumetiwa taji kwa Uzima wa Milele, nayo milki yetu ni dunia, “Kuwafanya makuhani na wafalme kwa Mungu.” Hiyo ni kweli. Kwa hiyo haya basi.

²⁴⁰ Basi huko Yerusalemu Mpya, jinsi ambavyo wafalme wa nchi watakavyoleta utukufu wao katika ule Mji kule. Loo, ni ajabu sana! Hebu . . . mkitaka kulichukua hilo. Mnaona, ni kama tu kung’aa kama nyota, taji. Nayo Danieli 12:3 inatoa sifa kubwa mno zake, endapo mngetaka kuliandika. Labda tungekuwa na wakati kwa dakika chache tu kulipata. Hebu tufungue Danieli, yale anayosema hapa, katika mlango wa 12 wa Danieli. Vema. Hebu tuanzie kwenye cha kwanza, mlango wa 12:

Wakati huo Mikaeli. . . (Mnaona? Loo, mnajua huyo ni nani!) . . . ata- . . . atasimama, jemadari mkuu asimamaye upande wa wana wa watu wako: na kutakuwako na wakati wa taabu, (Ni kitu gani? Mara baada ya hii. Dhiki!) . . . mfano wake haukuwapo tangu lilipoanza kuwa taifa mpaka wakati uo huo: na wakati huo watu wako wataokolewa, kila mmoja atakayeonekana ameandikwa katika kitabu kile.

Tena, wengi wa hao walalao katika mavumbi ya nchi wataamka, na wengine wapate uzima wa milele (ile taji), wengine aibu na kudharauliwa milele.

Na walio na hekima watang’aa kama mwangaza wa anga; na hao waongozao wengi kutenda haki wata- . . . kama nyota milele na milele.

²⁴¹ Loo, ndugu, hiyo hapo “Taji” yako, taji ile tukufu ya Uzima wa Milele! Taji ya Uzima wa Milele.

²⁴² Kifungu cha 12, upesi sana kabla ya sisi. . . Nami nafikiri tunaenda hapa baada ya hilo basi.

Yeye ashindaye nitamfanya kuwa nguzo katika hekalu la Mungu wangu. . .

243 Sasa tutapitia hili upesi sana kwa kuwa nimepitiliza wakati kwa dakika tano. Lakini mnaweza kulala zaidi kidogo asubuhi, sivyo? Mama, mwache alale. Wewe amka tu, ila Baba kidogo ni vigumu kuamka. Ila mwache tu alale kidogo zaidi. Ponyoka polepole sana, mpikie kahawa yake, ama chochote afanyacho, naye atakuwa mchangamfu.

Yeye ashindaye nitamfanya kuwa nguzo katika hekalu la Mungu wangu, . . .

244 Loo, hebu tulichukue tu neno kwa neno kwa dakika moja tu. Mtanivumilia muda mrefu hivi, kidogo tu? Ninajua kuna joto, nanyi mnajua ni joto hapa juu pia. Lakini hebu tuone:

. . . Mimi nitamfanya . . . Yeye ashindaye nitamfanya kuwa nguzo katika hekalu la Mungu wangu, . . .

245 “Nguzo.” Nguzo, ama “msingi.” Msingi katika hekalu la Nyumba, ama Nyumba ya Mungu. “Hekalu la Mungu wangu,” ama, “‘Nyumba’ ya Mungu wangu.” Ni nguzo, msingi. Hawa ni wale waliolichukua Neno walilosikia (katika kifungu cha 8), ndipo wakarudi kwenye ule msingi.

246 Sasa hebu tuchukue Waefeso 2:19, huko kwenye kanisa la Efeso. Mnajua, inawabidi kurudi kwenye Efeso, hiyo ilikuwa ndiyo mwanzo. Hiyo ni kweli? Vema, hebu turudi kwenye Efeso ambapo Paulo alikuwa, kanisa ambalo alianzisha. Basi hebu tuone mahali tulipo. Vema, kanisa la Efeso. Hebu turudi sasa tuone msingi huu ni nini kule nyuma, tuone kile Paulo alichosema kuhusu ule msingi huko nyuma kwenye wakati wa kwanza wa kanisa kule. Sasa yeye anazungumza na Waefeso:

Basi tangu sasa ninyi si wageni ama wapitaji, bali ni wenyeji pamoja na watakatifu, watu wa nyumbani mwake Mungu.

Mmejengwa juu ya msingi wa . . . (Kilutheri, ama wa—ama wa Kibaptisti . . . Sasa, ngojeni, nimechanganyikiwa, sivyo? Uh-ah.)

Bali mmejengwa juu ya msingi wa mitume na manabii, Yesu Kristo mwenyewe ni jive la pembeni;

247 Kila kitu kilipitia Mlangoni, Yesu! “Na yeye ashindaye nitamfanya kuwa nguzo.” Kwa maneno mengine, sehemu ya ule msingi. “Nitampa nini? Nitaweka ndani yake Fundisho la mitume na manabii tangu mwanzo, na kumpa Ufunuo.” Manabii walisema nini juu Yake? Yeye ni Mshauri, Mfalme wa Amani, Mungu Mwenye Nguvu, Baba wa milele. Hivyo ndivyo walivyosema, hao manabii, mitume. “Naye anayeweza kushinda masinagogi haya yote ya Shetani, ajiweke huru na kutazama moja kwa moja kwenye lile Lango, nitamfanya kuwa nguzo, nitamrudisha kwenye msingi wa Neno Langu katika Nyumba

ya Mungu Wangu.” Loo, jamani! “Nitamweka pale pale kwenye nguzo hiyo, kwenye msingi ambamo unakaa moja kwa moja katika Neno.” Amina. Ninapenda hilo, ndugu, Hilo ni zuri. Huenda nikatenda kigeni, mimi . . . bali najisikia vizuri. Vema.

. . . kumfanya . . . Yeye ashindaye . . . kumfanya kuwa nguzo katika hekalu la Mungu wangu, wala hatatoka humo tena kabisa: . . .

Ni kitu gani hicho? Ikiwa yeye ni nguzo, yeye hatoki tena kabisa. Yeye ni Bibi-arusi! Hiyo ni kweli.

²⁴⁸ Kama vile wakati wa Efeso ulivyokuwa, kama vile Paulo alivyowafundisha katika Matendo . . . Sasa, ngoja kidogo. Kama utakuwa nguzo . . . Nilikuwa na Andiko lingine hapa chini nililotaka kuwaletea kabla hatujamfikia Bibi-arusi. Sasa, kama yeye atakuwa ni nguzo, unarudi kwenye Efeso, unarudi nyuma kwenye ule wakati alimokuwamo Paulo. Naye Paulo, yule malaika wa Efeso, ambayo ilikuwa ndiyo mwanzo wa kanisa, ule msingi, yeye aliwafundisha, “Kama walibatizwa kwa njia nyingine yoyote mbali na Jina la ‘Yesu Kristo,’ ilibidi wabatizwe tena.” Hiyo ni kweli, Matendo 9, ama 5:19, ama 19:5, hasa. Katika Wagalatia 1:8, yeye alisema, “Kama malaika akifundisha lingine lolote, na alaaniwe.”

²⁴⁹ Walikuwa pia ni Bibi-arusi waliokuwa kwenye hekalu. Sasa hebu tufungue Ufunuo mlango wa 7, tuone kama walikuwa ni Bibi-arusi, mlango wa 7 wa Ufunuo.

²⁵⁰ Sasa, huenda, ni—ni . . . Tunazungumza hapa, masalia wa Israeli, mia moja na arobaini na nne elfu, na kadhalika, bali hebu—hebu turuke tu hayo kidogo tu tushuke hapa yapata kifungu cha 12. Aisee, ni mkutano wa kipentekoste hapo! Hao ndio wale watu ambao walikuwa . . . loo, mnaona . . . Vema, tutaanzia hapa kwenye kifungu cha 9 maana cha kwanza ni kwa Israeli, nako kulikuwa na mia moja na arobaini na nne elfu waliotiwa muhuri, ambao tutawafikia kesho.

Na . . . Baada ya haya nikaona, na tazama, mkutano mkubwa sana ambao hapana mtu awezaye kuuhesabu, . . .

²⁵¹ Sasa, kumbukeni, kutoka 4 hadi 8 ni Israeli, ambao walikuwa ni matowashi, wa walinzi wa hekalu. Mnaona, tutalipata asubuhi, Bwana akipenda. Sasa, Yeye, anawatia muhuri pale, makabila yote kumi na mawili. Wa kabila la Yuda, Yeye akawatia muhuri kumi na mbili; Rubeni, akawatia muhuri kumi na mbili; Wa kabila la Gadi, akawatia muhuri kumi na mbili; na Lawi; na Zabuloni; na Benyamini, kumi na mbili. Basi kuna makabila mangapi ya Israeli? [Kusanyiko linasema, “Kumi na mawili.”—Mh.] Vema, kumi na mbili mara kumi na mbili ni ngapi? Mia moja na arobaini na nne elfu. Nao wote walikuwa ni wana wa Israeli; Yohana aliwajua, kila mmoja, yeye alikuwa ni Myahudi.

Baada ya haya...loo, mkutano mkubwa sana ambao hapana mtu awezaye kuuhesabu, (Hawa hapa Wamataifa wanakuja.) watu wa kila taifa, . . . kabila, na jamaa, . . . lugha, wamesimama mbele ya Mungu na . . . mbele ya Mwana-Kondoo, wamevikwa mavazi meupe, wana matawi ya mitende mkononi mwao;

252 Hao ni hao maskini viumbe kule nyuma waliokufa (nao simba wakawala, na kila kitu kingine) kwa ajili ya Injili hii ya Roho Mtakatifu ambayo iliendelea kudondoka damu. Maelfu mara maelfu ya watoto wadogo huku vichwa vyao vimepasuliwa mitaani, na kila kitu kingine, hao hapo wamesimama! Wamevikwa mavazi meupe, na mitende mikononi mwao. Loo, jamani!

Wakilia kwa sauti kuu wakisema, Wokovu una Mungu wetu aketiye katika kiti cha enzi, na Mwana-Kondoo.

. . . Wokovu una Mungu wetu yule aketiye katika kiti cha enzi, . . . na Mwana-Kondoo.

Na malaika wote walikuwa wakisimama pande zote za kile kiti cha enzi na hao wazee, na za wale wenye uhai wanne, . . . wakaanguka kwa ninii yao. . . wakaanguka kifulifulu mbele ya kile kiti cha enzi, wakamsujudu Mungu,

253 Sikilizeni, endapo hamfikiri huu ni mkutano wa Kipentekoste:

Wakisema—wakisema, Amina; Baraka, . . . utukufu . . . hekima . . . shukrani . . . heshima . . . uweza . . . nguvu, zina Mungu wetu hata milele na milele. Amina.

254 Whiu! Inasikika kana kwamba walikuwa na mkutano wa kambi huko, sivyo? Uh-huh.

. . . mmoja wa wale wazee ambaye—ambaye akajibu, akaniambia, . . . ama akaniambia, Je, watu hawa waliovikwa mavazi meupe ni akina nani? na wametoka wapi?

“Sasa, wewe ni Myahudi, uliyajua makabila yote kumi na mawili. Sasa, hawa nao ni akina nani? Wametoka wapi? Wamevikwa mavazi meupe, wametoka wapi? Si wa kabila la Benyamini na hayo mengine. Hawa nao walio hapa ni akina nani?”

255 Ndipo Yohana akaninii sana . . . ? . . .

. . . Nikamwambia, Bwana wangu, wajua wewe. (“Li—limenishinda! Ni—ni . . .” Mnaona?) . . . Akaniambia, Hawa ndio wanatoka katika dhiki zile zilizo kuu, nao wamefua mavazi yao, kuyafanya meupe katika damu ya Mwana-Kondoo.

Kwa kuwa... *Kwa hiyo wako mbele ya kiti cha enzi cha Mungu, (ndani ya Nyumba) nao watamtumikia mchana na usiku katika hekalu lake, naye aketiye katika kiti cha enzi atatanda hema yake juu yao.*

(Ilionekana kana kwamba walikuwa na njaa kidogo, sivyo?) *Hawataona njaa tena, (Utukufu!) wala hawataona kiu tena, wala jua halitawapiga wala hari iliyo yote.*

Kwa maana huyo Mwana-Kondoo, aliye katikati ya kiti cha enzi, atawachunga, ... atawaongoza hata kwenye chemchemi za maji yenye uhai, na Mungu atayafuta ... machozi yote katika macho yao.

Huyo hapo; huyo hapo Bibi-arusi. Loo, jamani! Ni nzuri jinsi gani! Bibi-arusi!

²⁵⁶ Hebu tuone yale aliyosema hapa sasa, ili tuhakikishe hatutalikosa sasa, cha 12:

Yeye ashindaye atakuwa nguzo katika hekalu la Mungu wangu, wala ... hatatoka humo tena kabisa; ...

Bibi-arusi akisimama pamoja na Bwana-arusi. Loo!

²⁵⁷ Loo, loo, laiti tungalikuwa na wakati wa kuchukua niliyo nayo (ni kwa ajili ya kile kitabu kule); kwenye Ufunuo, liliposema, “Wafalme wote wa duniani wanaleta heshima yao kwake.” Hiyo ni kama ninii... (katika mfano) kabila la Lawi: hao wengine wote walimtolea zaka, mnaona; kutoka mwezi mmoja mchanga hadi mwingine, sabato moja hadi nyingine, walipanda kwenda kuabudu. Itakuwa ni siku ya jinsi gani! Vema. “Nami nitaninii...” Hebu tuone, “Hatatoka humo tena kabisa.” Vema:

...nguzo katika hekalu la Mungu wangu... nami nitaandika juu yake jina la Mungu wangu, ...

²⁵⁸ Sasa, jina la Mungu ni lipi? Yesu. Iwapo unataka kuliandika hili (Tunachelewa kidogo.), “Yesu!” Waefeso 3:15 ilisema, “Mbinguni na duniani, wote unaitwa Yesu,” mnaona. Vema. Vema, sasa. Vema:

...na jina la mji wa Mungu wangu, huo Yerusalemu mpya, ushukao kutoka Mbinguni kwa Mungu wangu: Nitaweka juu yake... (Loo! Kama ukiona, yote ni Jina lile lile, mnapaswa tayari kuwa mmelishika. Mnaona? Mnaona?)... Nitaweka juu yake... jina la mji wa Mungu wangu, ...

²⁵⁹ “Ule Mji.” Yeye anaendelea na kusema, “ambao ni Yerusalemu Mpya.” Mnaona, Yerusalemu Mpya. “Nitaweka juu yake Yerusalemu Mpya.” Sasa, Bibi-arusi, ama Kanisa, ndilo Yerusalemu Mpya. Ni wangapi wanaojua hilo? Kanisa lenyewe ndilo Yerusalemu Mpya. Mnaamini hilo?

260 Hebu tulithibitisha. Ufunuo 21, nafikiri ndipo, hapo ninapotaka. Vema, hebu tuangalie nyuma hapa tupate kuwaonyesha. Biblia ilisema, “Hakikisha mambo yote,” mnaona. Sasa, Ufunuo 21. Loo, sikilizeni haya . . . hili . . . sikilizeni hili, mnataka kuona Mji huu mpya Wake (Jina la Mungu) ni nini.

Kisha nikaona mbingu mpya na nchi mpya; kwa maana mbingu ya kwanza na . . . nchi ya kwanza imekwisha kupita, wala hapana bahari tena.

Na mimi Yohana nikauona mji ule mtakatifu, Yerusalemu mpya, ukishuka kutoka mbinguni kwa Mungu, umewekwa tayari, kama bibi-arusi aliyekwisha kupambwa kwa mumewe.

261 Lile Kanisa m—mpya ni Kanisa la Mataifa, Bibi-arusi. Bibi-arusi ni Mmataifa, naye Mmataifa ana Jina Lake. Yeye aliwatoa watu kutoka kwa Mataifa kwa ajili ya Jina Lake. Mnaamini hilo?

262 Endapo huamini hilo, fungua katika Matendo 15:14 upate kujua. Matendo 15:14, kama unataka kulifungua kwa sekunde moja tu, nasi tutaninii . . . kisha utaninii . . . Matendo mlango wa 15 na kifungu cha 14, ninaamini tutalipata. Sasa, tuko tu tayari kufunga. Matendo 15, na kifungu cha 14:

Na hao walipokwisha kunyamaza, Yakobo akajibu, akisema, Ndugu zangu, nisikilizeni:

Simeoni ametueleza jinsi Mungu hapo kwanza alivyowaangalia Mataifa ili achague watu katika hao kwa ajili ya jina lake.

Uh-huh. Vema, Huyo hapo. Loo!

263 Sasa nafikiri hilo ni karibu sana tumefikia mwisho wake, na sasa tutafunga katika kusema ya kwamba huyu ni Yeye.

. . . nami nitaandika juu yake jina la Mungu wangu, na jina la mji wa Mungu wangu, . . .

Ambalo ni mamoja: Yesu, Yesu, Yesu. Naye Bibi-arusi ameolewa na Yesu, inamfanya Bibi Yesu; na kadhalika, mnaona.

264 Wapo wanawake wazuri sana kwenye jengo hili usiku wa leo, wazuri sana, ila kuna mmoja wao ambaye ni wangu, yeye analo jina langu. Ninatumai mlilipata hilo. Yeye analibeba jina langu, vivyo hivyo na Bibi-arusi Wake. Vema:

. . . Nitaandika juu yake jina la Mungu wangu, . . . huo Yerusalemu mpya, ushukao . . . ama, jina la mji wa Mungu wangu, huo Yerusalemu mpya, ushukao kutoka kwa Mungu . . . kutoka mbinguni kwa Mungu wangu: na nitaandika juu yake jina langu jipya;

265 Afadhali niachane na hilo, sivyo? Vema. Angalieni, “yeye” hapo ni umoja. Sasa kama utarudi kwenye Ufunuo 2:17 kwa dakika moja tu, kulirudia tu kwa sekunde moja:

Yeye aliye na sikio na alisikie neno hili ambalo Roho ayaambia makanisa. Yeye ashindaye nitampa baadhi ya ile mana iliyofichwa, nami nitampa jiwe jeupe, na juu ya jiwe hilo limeandikwa jina jipya asilolijua mtu ila yeye anayelipokea.

266 Hivi hamumpendi? Yeye si ni wa ajabu?

Nampenda, nampenda
Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

267 Mnajua, ninapenda kuimba katika Roho baada ya mkutano ambapo una huku kukatakata na kadhalika. Nanyi je? Loo, jinsi ninavyopenda kuingia katika Roho basi. Neno! Mnaona, Neno limeanguka sasa, sasa kitu pekee linachohitaji ni unyevu. Mnaona, sifa kidogo, ndipo lianze kukua, mnaona. Loo, hivi hamumpendi? Hebu tuinue mikono yetu na kuuimba huo:

Nampenda, nampenda
Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.


268 Loo, hebu tuinamishe tu kichwa chetu na kusema: “Baba, tunakupenda. Tunakupenda. Loo, jinsi tunavyokupenda! Tunakushukuru, sana, Bwana. Loo, maskini mioyo ye—yetu ya kibinadamu haiwezi kuelelezea yale tunayohisi ndani yetu, jinsi ambavyo Wewe umetuosha katika Damu Yako Mwenyewe. Sisi tulikuwa wageni, Bwana. Tu—tuliycopenda mambo ya ulimwengu, nasi tu—tulivurugika kabisa huko nje katika mambo ya ulimwengu, Nawe ulishuka kwa njia ya neema Yako na kuinyosha mikono Yako ya thamani mitakatifu kwenye taka za dhambi tulimokuwa, ukatuokota, ukatuchagua, ukatuosha, ukatusafisha, ukaweka Roho mpya ndani yetu, na kuweka upendo wetu kwenye mambo yaliyo juu. Jinsi tunavyokupenda, Bwana!”

269 Katika wakati huu uliodanganyika, hata hakuna kitu kingine ulimwenguni kilichosalia kwetu, Bwana. Hakuna kitu kilichosalia kwa ajili ya ulimwengu, ni—ni—ni kwenye wakati wa mwisho. Tunaona kupitia Biblia, kila kipindi cha wakati kimekwisha. Sasa tuko katika mwisho, unaopita upesi. Haitachukua muda mrefu hata Yesu aje. Ee Mungu, iwashe moto mioyo yetu, usituache tusimame kimya. Nafikiri, yule Mtakatifu mashuhuri Paulo angefanya nini kama angalikuwa hapa usiku wa leo na kuona jinsi mambo yaliavyo? Jinsi ambavyo... Mtu huyo, wangemtia gerezani kabla hakujapambazuka, yeye angekuwa hapa nje akiwaambia watu wajitayarisha kwa ajili ya kuja kwa Bwana.

270 Katika saa hii, Bwana, wapo wengi walio wagonjwa kwa kuwa hizi hapa lesu na haja zilizowekwa hapa. Ninaomba ya

kwamba Wewe utamponya kila mmoja wao, Baba. Tunajua hiyo ni sehemu ya huduma Yako ambayo umeithibitisha pasipo kukosea kwamba ni ya Kweli, “ishara zikimfuata mwaminio.” Kutoka kwenye mwili wa Paulo walichukua vitambaa na lesa na kuwatumia wagonjwa; ndipo pepo wachafu wakawatoka, nao waliponywa kwa sababu hao watu walimwamini Mungu aliye hai. Tujalie tena usiku wa leo, Baba, ninapowakabidhi Kwako, kupitia Yesu Kristo.

²⁷¹ Na sasa, Bwana, ninaomba ya kwamba Wewe utazichukua nafsi zetu mkononi Mwako, ukatuoshe, utupige pasi, kwa kuwa ilisema Wewe “unakuja kwa ajili ya Kanisa lisilo na waa wala kunyanzi.” Jalia pasi yenye joto ya Roho Mtakatifu inyoshe makunyanzi yote kutoka kwetu, nasi tumeanikwa tayari kwa ajili ya kuja kwa Mwana wa Adamu.

²⁷² Sasa, Baba, tunaomba ya kwamba baraka Zako zikae juu yetu. Abudu pamoja nasi, Baba. Tunakuabudu. Tunasimama usiku wa leo na kukupa Wewe mioyo yetu. Sisi . . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] 

WAKATI WA KANISA LA FILADELFA SWA60-1210
(The Philadelphian Church Age)

MFULULIZO WA UFUNUO WA YESU KRISTO

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza Jumamosi jioni, tarehe 10 Desemba, 1960, katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2021 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org